# Nipashe
Alhamisi Septemba 3, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580327
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US







## Mambo muhimu 33 ndani ya malengo sita Ilani ya CCM

UKURASA 4

UKURASA 11

# Rungwe atoa kali nyingine

UKURASA 3





Mgombea mwenza wa kiti cha urais kwa tiketi ya CCM, Makamu wa Rais Samia Suluhu Hassan, akiwasalimia wananchi wa kijiji cha Mvomero, mkoani Morogoro jana, alipokuwa njiani akitokea Turiani kuelekea Morogoro Mjini kuendelea na mikutano ya kampeni za uchaguzi mkuu. **PICHA: OMR**



Mgombea mwenza wa urais kwa tiketi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Salum Mwalimu, akinadi sera kwa wananchi katika mkutano wa kampeni mjini Shinyanga jana. **PICHA: MARCO MADUHU**

## Askari 19 kizimbani tuhuma za mlungula

UKURASA 5

# JPM aahidi maajabu

• **Asema** mitano ijayo Tanzania kama Ulaya, Lissu, Membe watema cheche wakisaka kura...

*Endelea ukurasa 2*



Mgombea mwenza wa urais wa ACT-Wazalendo, Prof. Omary Kakhi Mohammed, akihutubia katika mkutano wa kampeni, Kilwa Masoko mkoani Lindi, jana. **PICHA: ENOCK CHARLES**




Scan Hapa
Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu
Google Play
App Store

Fursa kwa Wagombea! 2020
VOTE

Gazeti la Nipashe linawapongeza wateule wote waliopitishwa na vyama vyao kugombea ubunge katika majimbo mbalimbali nchini
Je ungependa kukishukuru chama chako ?
Je ungependa kutangaza sera zako kwa wapiga kura ?
Nipashe inatoa nafasi kutangaza sera zako kwa gharama nafuu

Nipashe
MWANGA WA JAMII
Wasiliana nasi
Simu: 0686 101335,
Barua pepe: advertise@guardian.co.tz
VOTE




Mlezi wa Kamati ya Amani ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni, jijini Dar es Salaam, Sarah Msafiri, akizungumza katika kongamano la viongozi wa dini lililofanyika Kigamboni, jana, kwa ajili ya kuiombea nchi amani katika uchaguzi mkuu ujao. Kushoto ni Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Sheikh wa Wilaya hiyo, Abdallah Iddy na (kulia) ni Makamu Mwenyekiti, Mch. Charles Chiswagala. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# JPM aahidi kufanya maajabu

**Na Gwamaka Alipipi,** NZEGA

MGOMBEA urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. John Magufuli, amewaomba Watanzania kumchagua tena, ili awaonyeshe kile alichokiita maajabu kwa maendeleo ya nchi.

Amesema dhamira yake ni kuhakikisha anaitengeneza Tanzania kuwa kama Ulaya kwa kufanya mambo ambayo yamefanyika kwenye nchi zilizoendelea.

Alitoa kauli hiyo jana wilayani Nzega mkoani Tabora alipohutubia wananchi waliojitokeza kwenye Uwanja wa Parking kumsikiliza.

"Nirudisheni tena miaka mitano muone maajabu tutakayoyafanya... ninasema kwa dhati mtaona maajabu. Ninataka kuitengeneza Tanzania kuwa Ulaya, treni mnazoziona Ulaya ninataka kuzileta Tanzania, ndege mnazopanda kwenda Ulaya ninataka mzipande hapahapa.

"Ulaya ninaijua vizuri sana, niliendа wakati ninasoma. Hata nilipoingia madarakani, sijawahi kukanyaga huko kwa sababu ninataka kuwatumikia Watanzania kwa dhati pamoja na kuwaletea yale mnayoyafuata huko Ulaya. Sasa nipeni miaka mitano muone maajabu yake," aliahidi. Dk. Magufuli alisema yuko radhi atukanwe matusi yote, lakini atahakikisha Tanzania inapata maendeleo ikiwamo katika sekta ya elimu, afya na miradi mingine muhimu ya maendeleo.

"Kazi yangu ni sadaka kwa ajili ya Watanzania, matusi ninayotukanwa ninafurahi, kila siku ninasema muendelee kuniombea maana wanaotuibia hawawezi kufurahi, ndiyo maana matusi yote yanakuja kwangu.

"Acha mimi nitukanwe lakini Watanzania wapate maendeleo. Leo (jana) nimekuja hapa (Nzega) kuomba tena kura," alisema Dk. Magufuli.

Kuhusu Mkoa wa Tabora hususan wilayani Nzega, Dk. Magufuli alibainisha kuwa katika kipindi cha miaka mitano ya uongozi wake, amefanikiwa kutekeleza mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria ambao unahudumia wananchi wapatao 55,000 wa wilaya hiyo.

Vilevile, alisema amefanikiwa kujenga wodi ya wazazi, kituo cha afya, wodi ya upasuaji kwa kinamama wajawazito na ujenzi wa zahanati tatu wilayani hapa.

"Tumejenga barabara kutoka Nzega-Tinde-Shinyanga pamoja na barabara itokayo Nzega-Tabora. Ni kazi nzuri iliyofanywa na marais walionitangulia. Huduma ya maji ilikuwa ni kilio, lakini leo kwa asilimia 95 maji yanapatikana," alisifu.

Aliongeza kuwa Sh. bilioni 600 zimetumika katika Mkoa wa Tabora kutekeleza miradi ya maji katika kipindi cha miaka mitano ya uongozi wake.

"Kuna watu wanaamini fedha zinatoka kwa wazungu tu na kwamba sisi Watanzania hatuna fedha, siyo kweli! Fedha zipo nchini, tena nyingi, mafisadi wamezikalia tu, sasa nichagueni tena nikamalizie pale paliposalia," alisema.

Dk. Magufuli alisema Ilani ya CCM 2020-2025 imegusa makundi maalum katika kuwaletea maendeleo wakiwamo wakulima, wafugaji, wavuvi, machinga na mama lishe.

Mgombea ubunge wa Nzega Mjini kwa tiketi ya CCM, Hussein Bashe, alimwomba Dk. Magufuli atakaposhinda katika uchaguzi wa mwaka huu, kutekeleza mradi wa ujenzi wa stendi ya mabasi, eneo la wafanyabiashara wadogo na mama lishe.

Bashe alisema Wilaya ya Nzega kwa sasa inakamilisha mradi wa uzalishaji wa mbegu wenye thamani ya Dola za Marekani milioni saba katika Bwawa la Kilimi.

"Mbegu za mahindi wakulima wananunua kwa Sh.12,000, mradi huu ukikamilika, bei itashuka hadi Sh. 5,000," alisema Bashe ambaye pia ni Naibu Waziri wa Kilimo.

Alibainisha kuwa kwa sasa kata zote za Wilaya ya Nzega zimeshafikiwa na huduma ya umeme na kinachoendelea ni kupeleka huduma hiyo katika vitongoji.

Alisema kwa muda wa miaka mitano, Halmashauri ya Wilaya ya Nzega imetekeleza miradi mbalimbali yenye thamani ya Sh. bilioni sita.

## Membe: Nitawapa uhuru watendaji

**Na Enock Charles,** KILWA

MGOMBEA urais kupitia Chama cha ACT Wazalendo, Bernard Membe, amesema iwapo atachaguliwa kushika nafasi hiyo, serikali yake haitaingilia majukumu ya watendaji wa chini yake.

Akizungumza katika kampeni yake mjini hapa jana, Membe alisema ili watendaji katika serikali wafanye kazi kwa ufanisi, wanapaswa kufanya kazi zao kwa uhuru bila kuingiliwa.

"Mfano kazi ya kuteua wakurugenzi ni kazi ya Waziri Mkuu na (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa) TAMISEMI si kazi ya Rais. Ukiwa unaingilia watendaji wa chini yako, matokeo yake Mkuu wa Mkoa anaweza kumdharau Waziri Mkuu," alisema Membe.

Alisema akiwa Rais, ataimarisha kuheshimiana baina ya watendaji na kuacha kila jukumu kufanywa na mtu atakayemteua katika nafasi hiyo huku akijinasibu kuwa atakuwa Rais wa wote si wa wanyonge au wenye nguvu pekee.

"CCM inasema yenyewe ya wanyonge, mimi nitakuwa Rais wa wote," alisema.

Membe pia aligusia miundombinu katika mikoa ya kusini akisema ataimarisha barabara za kuingia katika miji na wilaya za ambazo alisema haziko katika hali nzuri.

Kuhusu uvuvi, alisema atakapoingia madarakani atawapa uhuru wavuvi na kuwapiga marufuku viongozi wanaochoma nyavu za wavuvi.

Naye Mgombea Mwenza, Prof. Omari Faki, aliwaomba wananchi kukichagua chama hicho ili kuwapo na Muungano wa haki na kuheshimiana ndani ya Tanzania.

Katika kampeni hizo, wasanii wa muziki wa kazazi kipya, Ney wa Mitego na Timbulo, waliwaburudisha wapigakura waliofika kwenye mkutano wa jana. Makamu Mwenyekiti wa ACT Wazalendo (Tanzania Bara), Dorothy Semu, aliwaomba wanawake kukichagua chama hicho kuepuka kero ya maji na kuahidi kuwa iwapo wataingia madarakani, wanawake watapewa afasi za uongozi 50 kwa 50.

"Serikali iliyopita kuna mawaziri wanawake wanne tu, sisi tutateua wanawake katika kila nyanja," alisema.

# Lissu atangaza neema madini, kilimo

**Na Waandishi Wetu**

MGOMBEA urais kupitia tiketi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, ameahidi kuinua kipato cha wakulima na wafugaji nchini kwa kuboresha na kulinda maslahi yao ikiwa atachaguliwa kuwa rais wa nchi mwaka huu.

Katika uzinduzi wa kampeni za chama hicho Kanda ya Serengeti mjini Shinyanga jana, Lissu alisema atahakikisha anafanya mageuzi katika sekta hizo mbili, akiahidi kuwa serikali yake kutowakopa wakulima.

Mtaalamu huyo wa sheria alisema sera na taratibu zinazosimamia zao la pamba nchini kwa sasa siyo nzuri na zinamfanya mkulima wa zao hilo kuendelea kuwa maskini kutokana na kutolipwa kwa wakati.

Alisema kuwa endapo akiingia madarakani, atahakikisha uchumi wa mkulima wa zao la pamba unakua kwa kasi kwa kuwa bei itakuwa nzuri na hakutakuwa na kadhia ya kumkopa mkulima.

"Wakulima wa pamba wamenyanyasika sana, yaani mtu anauza pamba yake halafu anakopwa. Sisi CHADEMA tukiingia madarakani, hakuna kumkopa mkulima wa zao la pamba, kahawa wala korosho. Sisi ni kulipa mkono kwa mkono, nipe nikupe," alisema.

Kuhusu sekta ya mifugo, Lissu alisema sekta hiyo muhimu kwa sasa imesahaulika, hivyo itakuwa miongoni mwa zitakazoboreshwa wakati wa uongozi wake Ikulu.

Makamu Mwenyekiti huyo wa CHADEMA pia aligusia sekta ya madini ambayo alidai kwa sasa iko mbioni kufa kutokana na migodi mingi nchini kuishiwa madini.

Aliahidi kuwa akiingia madarakani, atahakikisha wananchi waliopisha uchimbaji wa madini katika maeneo mbalimbali nchini, wanalipwa fidia, akikumbusha waliokuwa wakazi wa Bulyang'hulu ambao alidai bado hawajalipwa fidia.

Awali, Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, aliwataka Watanzania na wafuasi wa CHADEMA kutoogopa kubandika mabango ya uchaguzi ya chama hicho kila eneo ambako kuna mabango ya CCM kwa kuwa wana haki ya kufanya hivyo.

Mnyika alimtaka Kamishna wa Kodi wa Mamlaka ya Mapato (TRA) kutoa tamko kuhusu agizo lililotolewa na TRA Wilaya ya Ilala kutaka mabango ya aina hiyo yalipiwe, kama ni la mamlaka hiyo au kulitengua mara moja.

"Na kama siyo maagizo yake, amchukulie hatua mara moja mkuu wa kodi pale Ilala ambaye alituagiza tulipie mabango yote ya CHADEMA yanayohusu kampeni," alisema Mnyika.

Alisema uamuzi wa CHADEMA ni kuendelea kuweka mabango na bendera katika maeneo yote ambako CCM wameweka mabango na bendera zao wakati huu wa kampeni za uchaguzi mkuu.

"Weka bendera, kuweka mabango mahali popote ambako CCM imeweka matangazo yao na hatutayalipia kodi kwa sababu ni haki yetu kufanya kampeni ya kuomba kura wakati huu wa uchaguzi mkuu," alisema.

■ **Imeandikwa na Marco Maduhu (SHINYANGA) na Mary Geofrey**

## Dk. Mwinyi arejesha fomu, CHADEMA, CUF wachukua

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MGOMBEA urais wa Zanzibar kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Hussein Ali Mwinyi, jana alirejesha fomu ya kuwania nafasi hiyo, huku akiahidi kufanya kampeni za kistaarabu.

Dk, Mwinyi ni kati ya wagombea 17 waliochukua fomu za kugombea nafasi hiyo kupitia vyama vyao vya siasa.

Mwinyi alikuwa mgombea wa kwanza kuchukua fomu hiyo fomu hiyo katika Ofisi za Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) Agosti 26, mwaka huu.

DK.Mwinyi alikabidhi fomu hiyo majira ya asubuhi kwa Mwenyekiti wa ZEC, Jaji mstaafu Hamid Mahmoud, hivyo kutakiwa kusubiri hadi Septemba 10, mwaka huu kwa ajili ya kuthibitishwa na ZEC kuwa mgombea rasmi.

"Nathibitisha kupokea fomu zako kwa ajili ya kuomba kuteuliwa kugombea nafasi ya urais wa Zanzibar...tunazihakiki zaidi hadi hapo utakapojulishwa tarehe 10 kwa ajili ya kutangazwa na kuthibitishwa rasmi," alisema Jaji Mahmoud.

Akizungumza na waandishi wa habari, Dk. Mwinyi alisema CCM itahakikisha inafanya kampeni za kistaarabu na za kisayansi.

Alivitaka vyama vya siasa kufanya kampeni za kistaarabu, ambazo zitazingatia amani na utulivu wa nchi.

Aidha, Dk. Mwinyi aliwapongeza wana CCM na wananchi waliomdhamini na waliotaka kumdhamini na kutambua dhamira yao njema walioionyesha kwake.

"Walionidhamini wametosha nathamini dhamira yenu njema kwangu, hivyo sasa kazi iliyobaki ni kuhakikisha Oktoba 28, mnajitokeza kwa wingi katika vituo vya kupigia kura ili tuweze kuunda serikali na kuwatumikia wananchi," alisema Mwinyi.

**WAGOMBEA CHADEMA, CUF WACHUKUA**

Wakati huo huo, wagombea wawili wa Chama cha Maendeleo na Demokrasia Chadema (CHADEMA) na wa Chama cha Wananchi (CUF) walichuchua fomu hizo na kufikisha idadi ya waliochukua kuwa 17.

Naye mgombea wa CHADEMA, Said Issa Mohamed, alisema iwapo akichaguliwa kuongoza Zanzibar, anakusudia kuimarisha sekta ya elimu na mageuzi yake kwa ajili ya kutoa wahitimu watakaoingia katika soko la ajira kwa mafanikio makubwa.

Aidha, alisema maslahi ya watumishi wa Serikali yataboreshwa katika kipindi cha uongozi wake ili kuleta ufanisi katika sehemu za kazi.

"Nikichaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar nakusudia kuimarisha sekta ya elimu kutoa wahitimu watakaoingia katika soko la ajira kwa mafanikio makubwa sambamba na maslahi ya watumishi wa Serikali kuwa bora," alisema.

Mgombea wa CUF, Mussa Haji Kombo, alisema endapo atapata ridhaa za wananchi atawaletea Wazanzibari maisha bora kwa kutumia rasilimali ziliopo nchini.

"Nimechukua fomu kuomba kuteuliwa kwa ajili ya urais wa Zanzibar...naahidi kuleta maisha bora kwa kutumia rasilimali ziliopo nchini," alisema.

Wagombea 17 waliochukua fomu hadi jana ni Dk. Hussein Mwinyi, Said Soud (AAFP), Juma Ali Khatib (ADA TADEA),Hamad Rashid (ADC), Mfaume Khamis (NLD, Ali Juma (CHAUMA), Issa Muhammed Zonga (SAU), Ameri Said Ameri (Demokrasia Makini) na Hamad Muhammed Ibrahim (UPDP).

Wengine ni Shafii Hassan Suleiman (DP), Khamis Faki Mgau (NRA),Maalim Seif Sharif Hamad (ACT Wazalendo), Othman Rashid Khamis (CCK), Hussein Juma Salim (TLP) na Mohamed Omar Baharia (UMD), Mussa Haji Kombo (CUF) na Said Issa (CHADEMA).



Mgombea wa urais wa Zanzibar kwa tiketi ya CCM, Dk. Hussein Mwinyi arejesha fomu ya uteuzi wa nafasi hiyo kwa Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC), Jaji mstaafu Hamid Mahmoud, jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Rungwe atoa kali nyingine ya mwaka

**Na Thobias Mwanakatwe**

MGOMBEA urais kupitia Chama cha Ukombozi wa Umma (CHAUMMA), Hashimu Rungwe, amesema kama wananchi watampa ridhaa ya kuwa Rais wa Tanzania, miongoni mwa mambo atakayofanya ni kuziuza ndege za nchi zilizonunuliwa hivi karibuni.

Vilevile, Rungwe amesema kusudio lake hilo litakwenda sambamba na kuyauza magari yote ya gharama kubwa yanayotumiwa na wakuu wa mikoa nchini. Mgombea urais huyo aliyepata umaarufu mkubwa kutokana na kauli mbiu yake ya lishe bora na ya uhakika kwa wananchi, alitoa ahadi ya 'kuzipiga bei' ndege na magari ya serikali alipohojiwa na kituo cha runinga cha ITV kwenye kipindi cha 'Dakika 45' kinachorushwa juzi usiku.

Alisema kama atafanikiwa kushinda kiti cha urais katika uchaguzi mkuu uliopangwa kufanyika Oktoba 28 mwaka huu, atafanya tathmini ya ndege hizo na ikibainika zimekuwa nyingi na hazina kazi yoyote ya maana, atauziuza.

Kuhusu magari ya wakuu wa mikoa, Rungwe alisema baada ya kuyauza, viongozi hao wataanza kutumia magari aina ya Land Rover ambayo alidai ni mazuri kwa kuwa yana viyoyozi na yanafika mahali popote.

Kwa sasa, wakuu wengi wa mikoa nchini wanatumia magari aina ya Toyota Land Cruiser VX V8, ambayo Rungwe anaona ni ghali na yanaigharimu nchi fedha nyingi.

"Nikiona hakuna ulazima wa hizi ndege na zimekaa tu pale zinangoja itokee bahati ya tenda Zambia, mimi nitaziuza," Rungwe alisema.

Hadi sasa, Tanzania ina ndege 11 ambazo zimenunuliwa katika uongozi wa serikali ya awamu ya tano.

Rungwe pia alisisitiza kaulimbiu yake ya lishe bora na ya uhakika kwa wananchi kama akichaguliwa, akisema wanafunzi wote wanapata chakula shuleni bila malipo kuanzia chekechea hadi kidato cha nne ili wasome vizuri.

"Nitahakikisha ubwabwa, ugali na kuku wanafunzi wanapata ili wawe na akili timamu. Hivi sasa unakuta mwanafunzi hajui hata kuandika barua, ninayoyazungumza sifurahishi watu, watu wanipigie kura waone vitendo," alisisitiza.

Hata hivyo, Rungwe alikiri kwamba hakuna serikali inayoweza kugawa chakula kwa wananchi wote, lakini sera ya chama chake inalenga zaidi wanafunzi. Alisema wananchi wengine watawekewa mazingira mazuri ya kupata chakula kwa bei nafuu.

"Sera yetu ni kujali wananchi ambao ndiyo wanaleta kodi, tutatoa ajira nyingi kwa wananchi kupitia sekta ya kilimo na kuboresha huduma za afya na miundombinu," alisema hidi.

Awali, katika mahojiano na Nipashe, Rungwe alisema amepanga kuzindua kampeni zake Jumamosi huku akiahidi kuwa siku hiyo, 'atamwaga ubwabwa' kwa wananchi wote watakaojitokeza kusikiliza sera za chama chake.

Alisema uzinduzi huo utafanyika Manzese eneo la Bakhresa jijini Dar es Salaam kuanzia saa 9:00 alasiri.

Tanzania Forest Conservation Group
Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania

**TANZANIA FOREST CONSERVATION GROUP**

**STATEMENT OF RECEIPTS AND EXPENDITURE FOR THE YEAR ENDED 31 DEC 2019**

This publication of the Statement of Receipts and Expenditure is made in accordance with regulation 13(a) of the Non-Government Organization Act (Amendments), Regulation 2018 which requires Non-Government Organizations receiving funds exceeding TZS 20 Million to publish bi annually the funds received and its expenditure.

| DETAILS | ACTUAL - TZS |
|---|---|
| **RECEIPTS** | |
| Opening fund balance | 1,638,493,842.00 |
| Disbursement from Donors | 6,254,504,093.00 |
| **TOTAL RECEIPTS FROM DONORS** | **7,892,997,935.00** |
| | |
| **PROGRAMMES EXPENDITURE** | |
| Research | 70,768,370.00 |
| Environmental Education | 340,821,360.00 |
| Community Development (Poverty reduction in rural communities) | 3,404,477,990.00 |
| Communication and Advocacy | 7,631,015.00 |
| **OTHER PROGRAMME EXPENDITURE** | |
| Institution Development and Resources Mobilization | 310,070,052.00 |
| Personnel | 1,968,006,359.00 |
| **TOTAL PROGRAMMES EXENDITURES** | **6,567,089,264.00** |
| **FUND BALANCE**** | **1,325,908,671.00** |

**Fund balance represents an obligation to conduct donor funded activities per contractual commitments made between donor/development partners and the organisation/recipient, where funds have not been transferred and such activities have not yet occurred.

**Executive Director**
**Tanzania Forest Conservation Group**
**Plot 323, Msasani Village**
**Mwaikibaki Rd**
**P.O. Box. 23410**
**Dar es Salaam**
**Tanzania.**

215883402

# Mambo muhimu 33 ndani ya malengo sita Ilani ya CCM

Na Salome Kitomari

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimejinasibu kwa malengo sita ya uchaguzi wa mwaka huu, huku kikieleza mambo muhimu 33 kwa kila lengo kuu.

Kwa mujibu wa Ilani ya CCM iliyosambazwa kwenye mitandao ya kijamii, malengo makuu hayo yamejikita katika maeneo mbalimbali.

Katika ukurasa huo imeelezwa kuwa maudhui ya ilani hiyo yamezingatia mwelekeo wa sera za CCM wa 2020-2030, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2020-2050.

Pia ilani hiyo imezingatia fursa na changamoto zinazotokana na mabadiliko ya kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiteknolojia yanayotokea chini na duniani, pamoja na madhara ya janga la corona.

**UTU, USAWA na HAKI**

Ilani hiyo imebainisha kuwa italinda na kuimarisha misingi ya utu, usawa, haki na uongozi bora ili kudumisha amani, umoja na mshikamano wa taifa na kuendelea kudumisha na kuimarisha umoja, udugu, mshikamano, amani, utulivu, ulinzi na usalama. "Kuendelea kuimarisha Muungano wa serikali mbili, kuenzi uhuru na nchi na Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar pamoja na kutumia tunu zingine za kitaifa ikiwamo falsafa ya Mwenge wa Uhuru katika kujenga moyo wa uzalendo na uwajibikaji," ilisema sehemu ya ilani hiyo.

**UCHUMI WA KISIASA**

Katika eneo hilo ilani inaelezea kukuza uchumi wa kisiasa, fungamanishi, jumuishi na shindani uliojengwa katika msingi wa viwanda, huduma za kiuchumi na miundombinu wezeshi.

Ilani hiyo ilibainisha kuwa lengo lingine ni kuendelea kujenga na kukuza uchumi shindani husuasan kupitia sekta za viwanda na huduma za kiuchumi utakaowezesha ustawi wa wananchi wote.

**MAGEUZI YA KILIMO**

CCM imeahidi kufanya mageuzi ya kilimo, mifugo na uvuvi ili kuwa na uhakika wa chakula na kujitegemea kwa chakula wakati wote na kuchangia kikamilifu katika maendeleo ya kiuchumi.

Ilani hiyo imejinasibu kuwa itaongeza uzalishaji katika mazao ya chakula, ufugaji na uvuvi kwa ajili ya kujitosheleza kwa chakula na lishe bora.

"Kuimarisha miundombinu na kuongeza maeneo ya umwagiliaji katika kilimo, ili kupata mazao mengi zaidi kwa ajili masoko ya ndani na nje ya nchi,"ilisema Ilani hiyo.

**HUDUMA ZA KIJAMII**

Katika huduma za kijamii, CCM imejinasibu kuimarisha upatikanaji wa huduma bora za afya, elimu, maji, umeme na makazi vijijini na mijini.

"Kuendelea kuimarisha mifumo ya elimu ili uweze kuzalisha wataalam mahiri zaidi wenye uwezo katika sayansi, teknolojia, ufundi na nyanja nyingine, ambao wanaweza kujiajiri na kuajiriwa ndani ya nchi na mahali popote duniani,"ilibainisha.

Aidha, jambo jingine ni kuhamasisha na kuweka mazingira wezeshi, ili wananchi katika maeneo yote nchini wawe na makazi bora.

**MATUMIZI YA UTAFITI**

Ilani hiyo inaelezea kuchochea matumizi ya utafiti, sayansi, teknolojia na ubunifu kama nyenzo ya maendeleo ya haraka ya kijamii na kiuchumi.

Pia imejipambanua kuwa itahuisha na kuimarisha taasisi za utafiti, sayansi, teknolojia na ufundi ili ziweze kubuni nyenzo za kuongeza tija katika sekta za uzalishaji na huduma.

AJIRA MILIONI NANE

Nyingine ni kutengeneza ajira zisizopungua milioni nane katika sekta rasmi na isiyo rasmi kwa ajili ya vijana.

Aidha, ilani hiyo imesisitiza kuchochea ukuaji wa uchumi hususan katika sekta ya viwanda, vinavyotumia malighafi za kilimo, mifugo, uvuvi, madini, maliasili na sekta ya huduma za kiuchumi ikiwa ni pamoja na utalii.

"Kuwawezesha vijana kushiriki katika shuguli za ujasiriamali, ikiwamo kuwapatia mafunzo na kuwaunganisha na taasisi na asasi za utoaji mikopo yenye riba na masharti nafuu," ilisema sehemu ya ilani hiyo.




Spika wa Bunge, Job Ndugai (wa pili kushoto), akipiga makofi baada ya kufungua jiwe la msingi la uzinduzi wa jengo la Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Wilaya ya Manyoni mkoani Singida, jana. Wa (pili kulia) ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Kapteni mstaafu George Mkuchika, Mkuu wa Wilaya ya Manyoni, Rahabu Mwagisa (kulia) na Mkurugenzi wa Uzuiaji Rushwa kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa taasisi hiyo, Sabina Seja. **PICHA: BUNGE**

# Balozi 10 zatoa tamko uchaguzi mkuu

Na Mwandishi Wetu

NCHI kumi zenye ofisi za ubalozi nchini, zimetoa tamko la kuitakia Tanzania mafanikio kwenye uchaguzi mkuu wa Oktoba, mwaka huu, huku wakitaka misingi ya demokrasia kuheshimiwa ikiwamo kuwa na uchaguzi huru na haki.

Balozi hizo, Ubelgiji, Canada, Denmark, Finland, Ujerumani, Ireland, Uholanzi, Norway, Sweden na Uswisi, zilitoa tamko hilo lililosambazwa kwenye mitandao ya kijamii na kwenye tovuti zao.

"Kwa ujumla wetu tunaeleza matumani yetu na matarajio ya mchakato wa uchaguzi kuwa utakuwa huru na haki. Tunaunga mkono mchakato wa kidemokrasia na utendaji wa taasisi wa kidemokrasia Tanzania," ilisema sehemu ya tamko hilo.

"Tunaamini wanaume na wanawake, vijana na wazee watakuwa na haki sawa kushiriki mchakato uliobaki. Kuboresha uwazi kupitia waangalizi wa ndani na nje, uandishi wa habari huru, kina na usiopendelea."

Liliongeza tamko hilo na kusisitiza kuwa:

"Tunatarajia uamuzi wa haki wa migogoro ambayo vitaimarisha uhalali wa mchakato mzima wa uchaguzi kati ya raia wa Tanzania."

Aidha, balozi hizo ziliwataka wadau wote kujitolea kuhakikisha mazingira salama kwa washiriki wote, kuheshimu sheria na kutopendelea kabisa taasisi na mamlaka zinazohusika na kusimamia uchaguzi.

"Kama wawakilishi wa nchi zetu tunakumbuka hamu yetu ya muda mrefu na msaada kwa maendeleo na demokrasia nchini Tanzania kulingana na uhusiano wetu wa kihistoria na wa karibu," ilisema sehemu ya tamko hilo.

## Majaliwa aomba kura zote kwa JPM

Na Cynthia Mwilolezi, MONDULI

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewaomba wananchi wa mkoa wa Arusha kumchagua Rais John Magufuli na wagombea wake wote wa ubunge na udiwani wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), ili waendelee kuleta maendeleo zaidi ya sasa waliyoyafanya ambayo dunia inashuhudia.

Akizungumza jana Mto wa Mbu wilayani Monduli, wakati akimnadi mgombea ubunge wa jimbo hilo, Frederick Lowassa, na Rais Magufuli, alisema ni vyema wapigakura wakachagua viongozi bora kupitia chama hicho na si vinginevyo.

"Sina mashaka (shaka) mtatupa kura zote kwa sababu serikali imefanya makubwa kama vile tumejenga vituo vya afya 498 nchini na vyote vina jengo la upasuaji na tumewapunguzia safari za kufuata huduma hizo mbali au wilayani," alisema.

Majaliwa alisema kila wilaya vimejengwa vituo hivyo na bado wanahitaji kuongeza vituo hivyo, lakini wanahitaji kupata kura zote ili watekeleze hilo. "Leo (jana) nitakabidhi Ilani ya CCM ili wananchi waone kazi tutakazozifanya, sasa naomba Fredrick beba kero zote za wananchi ili ukashughulike nazo," alisema.

Mbali na ujenzi wa vituo vya afya, pia alisema wanajenga hospitali za wilaya na wanaendelea kujenga katika wilaya zote na kwamba serikali imeshatoa zaidi ya Sh. bilioni 2.5 za dawa kwenye hospitali na vituo vya afya, hivyo wanaomba kura ili waendelee kukamilisha waliyodhamiria.

"Muhimu zaidi mjue tumedhamiria kusomesha watoto wetu kuanzia chekechea hadi chuo kikuu. Mnajua tumefuta michango ya ovyo ovyo shuleni leo mtoto anakwenda shuleni bila malipo ili zile fedha mlizokuwa mnatumia kwa michango, mtumie kwa mambo mengine," alisema.

Katika kufanikisha hilo, alisema kila mwezi zaidi ya Sh. bilioni 24 zinatengwa kwa ajili ya shule za msingi na sekondari na pia wanapeleka fedha nyingi ili watoto wasome bila shida.

Alisema hata vijana wanaokwenda vyuo vikuu wamepanua wigo wa utoaji mikopo kutoka Sh. bilioni 350 hadi sasa zaidi ya Sh. bilioni 400 ili vijana wasome bila kukwama. "Hapa Monduli tumeleta Sh. bilioni 12.9 miradi ya vijijini ili wachimbe visima japo maji mengi yapo ila hayafai kwa kunywa sababu yana madini yasiofaa kutumika ila tunahangaika kutafuta vyanzo vya maji na ndio hizi fedha tumeleta," alisema.

Alisema lengo kumwondolea mama mzigo kichwani na vijana kuhangaika kutafuta maji na madumu badala ya kufanya shughuli za uchumi.

Kuhusu uboreshaji barabara serikali imetoa Sh. bilioni 2.37 ili barabara zitengenezwe wilayani humo na kurahisisha usafiri.

HABARI KITAIFA

# Askari wanyamapori 19 kortini madai kuomba, kupokea rushwa

**Na Happy Severine,**
SIMIYU

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Simiyu kwa kushirikiana na Kikosi Kazi Taifa Dhidi ya Ujangili, imewafikisha mahakamani askari 19 wa wanyamapori kwa tuhuma za rushwa.

Watuhumiwa hao wakiwamo askari wa Mamlaka ya Hifadhi ya Wanyamapori Tanzania (TAWA), wanatuhumiwa kuomba na kupokea rushwa ya Sh. milioni 70.4 kutoka kwa wafugaji wa maeneo ya Itilima mkoani hapa.

Kati ya watuhumiwa hao 19, watatu ni watumishi wa kampuni ya uwindaji ya Fredikin Conservation Fundi (FCF).

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Simiyu, Joshua Msuya, alisema watuhumiwa hao walisomewa mashtaka ya kuomba na kupokea rushwa mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi wa Mkoa wa Simiyu, Venance Mlingi.

Alisema watuhumiwa hao walisomewa kesi tano za rushwa tano ambazo kati ya hizo tatu ni namba 14, 15 na 16 za mwaka 2020 chini ya Hakimu Mlingi na kesi mbili namba 17 na namba 18 mbele ya Hakimu Marry Nyangusi. Mwendesha Mashtaka wa TAKUKURU, Kelvin Murusuri, alidai kuwa kati ya Aprili Mosi na Juni 30, mwaka huu, watuhumiwa hao kwa tarehe tofauti, kwa pamoja walikamata watu na mifugo yao waliyokuwa wakiichunga ndani ya pori la akiba la Maswa na kuwaomba rushwa ili wasiwachukulie hatua za kisheria.


"Watuhumiwa kwa pamoja na kwa nyakati tofauti waliwaomba watu hao rushwa, ili wasiwachukulie hatua kwa kuwa walikuwa wakichunga ndani ya hifadhi la pori la Maswa na waliomba kupewa Sh. 30,000 hadi 70,000 kwa kila kichwa cha ng'ombe waliokamatwa," alidai.

Mwendesha mashtaka huyo alidai kuwa katika mashtaka waliyosomewa, watuhumiwa waliomba na kupokea Sh. milioni 70.4 kutoka kwa wafugaji waliokamatwa.

Watuhumiwa walisomewa mashtaka ni James Chacha, Janeth John, Derick Mboneko, Baraka Lunengo, Anthony Hosea, Henry Kwambaza, Hombo Bajuta, Joseph Pius, Flavian Magabari na Kelvin Jackson.

Wengine ni Chacha Mwita, Magomba Mkaka, Juma Peter, Yohana Mkanzabi, Omari Katongari, Elibert Temba, Leonard Kileo na Maridadi Maridadi.

Watuhumiwa wote walikana mashtaka na wamerudishwa rumande baada ya kukosa dhamana na kesi zao zimeahirishwa hadi Septemba 15 na 19 kwa ajili ya kuanza kusikilizwa baada ya upelelezi kukamilika.




Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Doto James (katikati), akipokea mfano wa hundi ya Sh.bilioni 18.99, kutoka kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Airtel Tanzania, Gabriel Malata, ambayo ni sehemu ya Sh. bilioni 32.9 ambazo Airtel imeilipa Serikali ikiwa ni gawio na michango ya maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Serikali yapokea gawio la bil. 33/- kutoka Airtel

**Na Ibrahim Joseph,**
DODOMA

SERIKALI imepokea kiasi cha Sh. bilioni 32.99, likiwa ni gawio na mchango kutoka kampuni ya simu za mkononi ya Airtel Tanzania.

Makabidhiano hayo, yalifanyika jana jijini Dodoma, ambapo Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Dotto James, alipokea kwa niaba ya serikali.

Akizungumza wakati wa kukabidhi hundi, Mwenyekiti wa Bodi ya Airtel Tanzania, Pascal Malata, alisema kiasi hicho cha fedha ni sehemu ya faida iliyopata kampuni.

Malata alisema Sh. bilioni 18.99 zimetolewa kama gawio serikalini kutokana na kuwa na hisa za asilimia 49, Airtel ikibaki kumiliki hisa za asilimia 51 kwenye kampuni.

Alisema pia Airtel metoa Sh. bilioni 14 ukiwa mchango wa kampuni kwa jamii katika maeneo ya kutoa huduma mbalimbali. Alifafanua kuwa mchango pamoja na gawio vyote vina kamilisha kiasi cha Sh. milioni 32.99 kwa serikali.

Aidha, alisema Airtel Tanzania imetoa ajira 500, za moja kwa moja na zingine 350 kwa wauza vocha na mawakala kote nchini.

Alitaja mafanikio mengine ni mkataba walioingia na Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) ya kutoa elimu ya mafunzo mbalimbali kwa njia ya mtandao.

Kadhalika, alisema mfumo huo wa kutoa mafunzo kwa njia ya mtandao umewezesha vijana 17,493 kupata mafunzo hayo ambapo wanafunzi 500, wamehitimu kwa kusoma kwa njia hiyo.

Msajili wa Hazina, Athumani Mbutuka, alisema gawio hilo ni matokeo ya serikali katika kuisimamia kampuni hiyo ambayo ilikuwa haitoi gawio miaka ya nyuma tangu kuanzishwa kwake mwaka 2001.

Mbutuka alisema mwaka 2014/2015, serikali ilipokea kiasi cha Sh. bilioni 161, likiwa ni gawio kutoka taasisi mbalimbali.

Kadhalika, Mbutuka alisema katika mwaka wa fedha 2018/2019, serikali ilipokea zaidi ya trilioni 1, likiwa ni gawio na michango kutoka taasisi mbalimbali ambazo inahisa zake.

James aliishukuru kampuni hiyo kwa kutoa gawio kubwa kuliko taasisi zote za serikali.

Alizitaka taasisi zingine ambazo serikali imewekeza hisa zake kuhakikisha zinatoa gawio serikalini ili kutoa huduma za kijamii.

Alizitaka taasisi ambazo hazijatoa gawio serikalini mwaka huu, kujitathmini na kutoa.

# Wizara yamulika mitaala elimu ya juu

**Romana Mallya**

WIZARA ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi, imetoa wito kwa vyuo vikuu na taasisi za utafiti kujielekeza kwenye utafiti wenye lengo la kujenga msingi wa uchumi wa viwanda, kuwaandaa vijana na kuongeza thamani ya bidhaa viwandani.

Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Dk. Leonard Akwilapo, alisema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa ufunguzi wa maonyesho ya 15 ya vyuo vikuu yaliyoandaliwa na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU).

Dk. AKwilapo alivitaka vyuo vikuu kuanzisha programu za masomo zinazoendana na rasilimali zilizopo pamoja na kuboresha maisha ya Watanzania kupitia sekta za mafuta na gesi, kilimo na afya.

Alivitaka vyuo na watafiti kujielekeza kwenye utafiti wa teknolojia na bidhaa za viwandani, kilimo, mifugo, uvuvi maliasili za misitu, utalii na madini.

Julai Mosi, mwaka huu, alisema Tanzania ilitangazwa rasmi kuingia katika uchumi wa kati ikiwa ni ndoto ya serikali ya awamu ya tano inayobainishwa katika dira ya maendeleo kuelekea 2025.

Alisema ni jukumu la vyuo kuhakikisha kwamba wanaendelea kujenga uchumi shindani kupitia shughuli za viwandani, mashambani na migodini ili bidhaa zitakazozalishwa ziweze kukidhi viwango vya ubora katika masoko ya nje.

"Uboreshaji huu bila shaka utahitaji elimu bora na inayoendana na wakati, hili ndilo agizo langu kwenu hakikisheni bidhaa zetu zinaendelezwa, zinapewa ubora zaidi ili zinapouzwa nje ziwe na thamani kubwa badala ya kuuza malighafi," alisema.

Dk. Akwilapo alisema ni jukumu la vyuo vikuu kuhakikisha katika utendaji wao wa kazi wanafanya utafiti za kuona kwamba wanaongeza thamani ya bidhaa zinazozalishwa Tanzania.

"Uboreshaji huu utahitaji elimu bora inayojikita katika fani mbalimbali, kupitia utafiti angalieni namna ya mtakavyoboresha elimu mnayoitoa ili kuleta tija katika taifa hasa katika eneo la uzalishaji mashambani na viwandani.

"Dhamira yetu ni kuwa na nguvu kazi iliyoelimika na yenye ujuzi wa kutosha wenye kubuni miradi mikubwa, ipo ambayo inayoendelea ujenzi wa reli ya kisasa, bwawa la Mwalimu Julius Nyerere, usafiri wa anga unaimarishwa, bomba la mafuta, tunahitaji wasomi wa kuiendesha na kuisimamia."

Alisema ni jukumu la taasisi za elimu ya juu kuhakikisha hili linafanyika kwa ufanisi wa hali ya juu katika kutengeneza rasilimali watu inayokidhi mahitaji kwa sasa.

Alisema baadhi ya vyuo vimejielekeza katika kutoa elimu inayoshughulikia changamoto za jamii na kuweka msisitizo kwenye maeneo ya kimkakati.

"Nisingependa kuona tunapeleka wagonjwa nje ya nchi kutibiwa, nchi hizo zilete wagonjwa Tanzania, vituo vingi vya utoaji tiba sasa vinapokea wagonjwa kutoka nje, tuendelee kuviimarisha," alisema.

Pia alizitaka taasisi za elimu ya juu zitafute namna ya kupanua udahili wa wanafunzi kwa sababu katika ngazi ya msingi na sekondari wameongezeka hivyo ni wazi miaka michache ijayo kutakuwa na idadi kubwa vyuoni.

Katibu Mtendaji wa TCU, Prof. Charles Kihampa, alisema lengo la maonyesho hayo ni kutoa fursa kwa taasisi zinazoshiriki kuzitangaza kazi mbalimbali wanazofanya na wanafunzi kuweza kujisajili.

Alisema taasisi 67 zimeshiriki kwenye maonyesho hayo zikijumuisha zinazotoa mafunzo ngazi ya elimu ya juu.

Kuhusu wakala wanaofanya usajili wa wanaotaka kwenda kusoma vyuo vya nje, Prof. Kihampa amewataka kufuata vigezo na taratibu kuhakikisha vijana wanaopata nafasi hizo hawaendi vyuo ambavyo havitambuliki.

Mwenyekiti wa Kamati ya Wakuu wa Vyuo (CVCPT), Prof. Raphael Chibunda, ambaye ni Makamu Mkuu wa Chuo wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, (SUA), aliihakikishia serikali kuyafanyia kazi yote waliyoelezwa.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kampeni zisiwe jukwaa la kuwatusi wanawake

**KAMPENI** za uchaguzi zimeanza na vyama mbalimbali vya siasa vinazunguka mijini na vijijini kunadi sera zake ambazo vinaamini vitawainua wapigakura kuwachagua kwenye ubunge, udiwani, uwakilishi na urais kwa kipindi cha miaka mingine mitano ijayo.

Kila chama kinazunguka maeneo mbalimbali kunadi sera zake, mikakati, malengo na mipango itakayotekelezwa kufanikisha maendeleo ya wananchi kuanzia sasa hadi 2020.

Hivyo ni jukumu la kila anayesikiliza sera hizo kufanya maamuzi sahihi na kuchagua chama anachokipenda na kiongozi anayeamini atatimiza haja za moyo wake.

Hata hivyo, katika kujinadi na kukitangaza chama haipendezi kuanza kutukana na kukejeli maisha binafsi ya wagombea hasa wanawake.

Aidha, tunaona kuwa kura ni mchakato unaohusu wadau wengi kuanzia vyama,wagombea, wapigakura, wanasiasa, wanahabari, wadau wa maendeleo na Watanzania kwa ujumla. Kwa hiyo suala la msingi linalotakiwa kuusimamia uchaguzi huu ni uvumilivu wa kisiasa kwani kila chama kina haki ya kujinadi na kutangaza sera zake, bila kuja ni chama tawala au cha upinzani.

Ikumbukwe hakuna maana kuwa na kampeni zinazojaa kukashifiana na kushindwa kuvumiliana hasa kutokana na ukweli kuwa ni lazima katika siasa kuwe na kuvumiliana, kutofautiana, kukubaliana kutokukubalia na vyote ni kwa ajili ya ulinzi wa amani na heshima ya kila mmoja wakati wa uchaguzi.

Tunasema haya kwa sababu kuna baadhi ya wapiga kampeni wamekuwa wakiwatukana wagombea na kuongea matusi na maneno ya kuudhi ambayo hayavumiliki dhidi yao. Inasikitisha kusikia maneno kama mwanamke fulani ni kahaba. Ameolewa na mumewe anatajwa jina na familia nzima inakashifiwa jukwaani.

Ikumbukwe kuwa kila msikiliza sera angependa kusikia mambo yanayomgusa siyo habari za uhusiano wa mke na mume wala kashifa dhidi ya wanawake.

Kadhalika, kila mtu ana haki ya kuishi maisha yake, lakini kulindwa utu wake na si kutumia mgongo wa chama kuwa hata ukitukana utalindwa. Ikumbukwe huna haja ya kuudhi wengine kwa sababu siasa siyo vita.

Tunaona kuwa hata kama una nia ya kummaliza mpinzani wako tumia njia bora zaidi kuliko kutegemea matusi na mambo ya nguoni hasa yanayohusu uhusiano wa mke na mume.

Ni dhahiri kuwa haina maana usikilize sera za kutukanana au kugombana na familia ya mwanasiasa fulani. Muda ni kitu cha thamani wagombea walenge kuwaeleza wapiga kura masuala yenye maudhui ya maendeleo na kuheshimiana badala ya kuwachamba kwa matusi ya nguoni, kashfa na maudhi.


Tunaamini kuwa zama hizi si za matusi ni za uvumilivu wa na ukomavu wa kisiasa. Kwa kuwa wanaochagua ni wananchi ambao ndiyo wanaofuatilia sera zenu wagombea ni vyema mkawapa kila wanachotaka badala ya kile mchopenda.

Ni vyema mchakato wa uchaguzi ukawa wa kufurahia badala ya kusababisha wagombea na wapigakura kupata maradhi kama shinikio la damu au au kiharusi kutokana na kukashifiwa ama kudhalilishwa majukwaani.

Baadhi ya wagombea wana hasira, maneno makali na hata chuki binafsi dhidi ya wapinzani wao. Yote hayo wayavumilie kutokana na ukweli kuwa uchaguzi unahitaji kuvumiliana na kuheshimiana pamoja na kukubaliana kutokukubaliana.

Pengine ni wakati wa kusimama majukwaani na kuwapa wapigakura vipaza sauti ili muwasikilize waeleze kile ambacho wanataka muwafanyie badala ya wagombea kuendelea kutoa maneno ya kashfa dhidi ya wale wanaowapinga.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Jitihada hizi zinaweza kukomesha uchafu Dar

Na Sabato Kasika

**DAR ES SALAAM** linaweza kuwa jiji safi Afrika na pengine dunia nzima iwapo sera ya kurejeleza taka ngumu Dar es Salaam itafanikiwa.

Sera hiyo inataka kuhakikisha wananchi hawaishi katika umaskini, bali wanakuwa na kiwango bora cha maisha na jiji lenye mazingira ya kiushindani yanayovutia wawekezaji.

Kwa mkakati huo, ni vyema sera hiyo ikaja na majibu ya kudumu ya kuliweka jiji kwenye usafi na ikiwezekana, taka ziwe zinakusanywa pamoja na kuzolewa kwa wakati na kubadilisha hali ilivyo sasa.

Jiji limekuja na sera hiyo, huku tatizo la kutupa taka likiwa ni kama jambo la kawaida, kukuta takataka barabarani ama katika mitaro na kwenye maeneo mengine, ambazo huzalishwa na wachuuzi na nyingine kutoka nyumbani'. Si hivyo tu maji taka yanachirizika ovyo wakati mitaro imegauzwa kuwa maeneo ya kukojolea na kutupa taka za vyooni kikiwamo kinyesi.

Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam, Sipora Liana, anaeleza katika utangulizi wake kuhusu sera hiyo kwamba, mazingira safi ni kitovu cha afya bora na maendeleo kwa wananchi.

Hivyo, kitovu hicho ni muhimu kiendelee kuboreshwa, kwa kuwa usimamizi endelevu wa usafi ni kuweka misingi ya usimamizi, tathmini na kuchukua hadhari kuhusu madhara kwa mazingira na afya za watu ikiwamo kudhibiti taka kuanzia zinapozalishwa, kuzikusanya, wakati wa kusafirisha na kuzirejeleza.

Mkurugenzi huyo anatambua kuwa njia mojawapo za kudhibiti taka ngumu ni kuzirejeleza ili kupata matokeo mazuri ni lazima kuweka misingi ya utekelezaji ikiwa ni pamoja ushirikishwaji umma.

Anabainisha kuwa, nchi zilizoendelea, zimegundulika kwamba ni hatari na hasara iwapo taka zote zitatupwa mahali pamoja na kufunikwa bila kurejelezwa, kwa vile ndani ya taka kuna thamani kubwa kiuchumi.

Kwa kutambua hilo, jiji limekuja na sera hiyo ikilenga kutenganisha taka na kuzikusanya kila aina ya taka peke yake na kwamba kwa mbinu ya kurejeleza wanaweza kuhifadhi maliasili na kuzalisha nishati kwa njia mwafaka zaidi.

Ni ukweli kwamba, kuzagaa kwa takataka mbalimbali kwenye baadhi ya maeneo ya jiji, kunasababisha liwe chafu, kwa vile zimo zinazochafua mazingira na pia kuhatarisha afya za wakazi wake.

Zipo sababu kadhaa zinazotajwa kuchangia kutupa taka ovyo jijini ikiwamo watu kutotambua madhara yake, kutojua kuwa vitendo hivyo vinawaathiri watu wengine na mazingira.

Uongozi wa jiji unakiri kutambua ongezeko la aina tofauti za taka ngumu zikiwamo zinazotoka 'majumbani', viwandani na hospitali, zinazotupwa maeneo mbalimbali na kusababisha uchafuzi wa mazingira.

Jambo la msingi katika yote hayo, ni sera hiyo kutiliwa mkazo ili isaidie kumaliza tatizo hilo, ambalo linatishia afya za watu na pia uchafuzi wa mazingira.

Ninatambua juhudi mbalimbali zinazofanywa za kuhakikisha jiji linakuwa safi, zikiwamo za aliyekuwa Mkuu wa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda za kuweka vijana waliomaliza mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) na mgambo kusimamia usafi na kuwatoza faini vinara wa uchafuzi wa mazingira.

Huo ulikuwa ni ubunifu mkubwa aliofanya Makonda katika kutatua tatizo la uchafuzi wa mazingira na kulifanya jiji kuwa katika hali ya usafi, ingawa juhudi hizo ni kama ziliishia njiani, na muhinu ukaboreshwa.

Vilevile, inaelezwa kuwa, kwa siku nyingi, jiji linazalisha taka tani 4,600 na asilimia 20 hadi 40 ndizo huzolewa na kupelekwa dampo Pugu Kinyamwezi, huku asilimia 60 inayobakia inasababisha jiji kuwa na taka kila kona.

Hali ya usafi hasa udhibiti taka ngumu ni tatizo la muda mrefu ambalo lina changamoto nyingi, kutokana na jamii kutozingatia usafi wa mazingira katika maeneo mbalimbali ya jiji.

HABARI KITAIFA

# Samia aahidi huduma bora zaidi za jamii

**Na Christina Haule,** MOROGORO

MGOMBEA mwenza wa urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Samia Suluhu Hassan, ameahidi kwamba kama chama hicho kitachaguliwa tena kushika dola, kitaendelea kutoa huduma muhimu kwa wananchi zikiwamo elimu, afya na maji.

Alisema kwa mujibu wa ilani ya CCM ya mwaka 2020-25 kama watachaguliwa, wamejipanga kuendelea na kazi ya kutoa huduma hizo kwa wananchi. Samia alisema hayo jana wakati akiomba kura kwa wananchi kwa ajili ya CCM kwenye uwanja wa Jamhuri Manispaa ya Morogoro.

Alisema wataendelea kutoa huduma za elimu, afya, maji, umeme na uwezeshaji jamii kiuchumu, mambo yatakayofanya uchumi kukua zaidi kuliko miaka mitano iliyopita.

Alisema pia wataendelea kutoa mikopo kwa wajasiriamali na kuendelea na ujenzi wa viwanda vilivyopo nchini ukiwamo Mkoa wa Morogoro. Kadhalika, alisema wamejipanga kukuza utalii kupitia bwawa la kuzalisha umeme katika mradi wa Mwalimu Nyerere baada ya kuweka mandhari nzuri ya bwawa hilo sambamba na kujenga barabara ya Morogoro - Kisaki kwa kiwango cha lami.

Vilevile, alisema ujenzi wa reli ya kisasa unaendelea, na kwamba wataendelea kufufua reli za ndani ya mikoa zilizokufa na wameshaanza za mikoa ya Kilimanjaro na Arusha.

Aidha, alisema watafufua viwanda vilivyopo mkoani Morogoro ili kuendelea kukuza uchumi wa watu na Taifa kwa ujumla.

Katika hatua nyingine, aliwataka wanachama wa CCM Mkoa wa Morogoro, kuwa wamoja na kufanya umoja huo utawale katika kipindi cha uchaguzi ili kufanya uwe wa amani.

Samia alisema kama wana-CCM wana ugomvi, basi wauache kwa sasa na kuendelea na masuala ya uchaguzi. Alisema ushirikiano unaotakiwa kwa sasa ni kuweka amani na utulivu, na viongozi kuweka usawa wa maendeleo ya nchi.




Naibu Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Dodoma, Manyama Tungazara (kushoto), akikabidhi fedha kiasi cha Sh. milioni 5.5 kwa mtumishi mstaafu Jumanne Muryery jijini Dodoma jana, alizokopeshwa kwa riba ya mkopo umiza toka kampuni ya Kihegha Investment Co. Ltd. **PICHA PETER MKWAVILA**

# IAA yapata dawa tatizo la ajira

**Na Mary Geofrey**

CHUO cha Uhasibu Arusha (IAA), kimeboresha mitaala yake ya elimu kwa lengo la kuwezesha wahitimu kujiari na kukuza uchumi wa taifa badala ya kutegemea kuajiriwa.

Mkuu wa IAA, Profesa Eliamani Sedoyeka, alitangaza neema hiyo jana katika maonyesho ya taasisi za elimu ya juu yaliyoandaliwa na Tume ya Vyuo Vikuu (TCU) kwenye viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam.

Alisema kuwa katika chuo hicho wameanzisha mafunzo ya ujasiriamali kwa wanafunzi wote, akibainisha kuwa walimu wanaboresha mawazo ya kibiashara yanayoibuliwa na wanafunzi ili vijana wajitegemee kwa kuanzisha miradi yao mwenyewe.

“Kwa mfano, sisi kipindi lilipotokea janga la corona, sabuni na sanitizer tulikuwa tunatengeneza wenyewe, hivyo tushaanza kuona mafanikio ya chuo chetu na kutatua tatizo la ajira nchini,” alisema Profesa Sedoyeka.

Alisema chuo chao pia kinawachukua wanafunzi na kuwakutanisha na vyuo vingine kwa ajili ya kubadilishana uzoefu na kupata mawazo mapya katika kuwajengea wigo mpana wa kujitegemea.

“Kwa miaka mingi baada ya uhuru, vyuo vingi vilikuwa vinatoa wanafunzi kwenda kujaza nafasi za kazi katika maeneo mbalimbali nchini, lakini kadri muda unavyozidi kwenda, nafasi zinazidi kuisha.

“Hivyo, tunawaandaa vijana kuwa katika mfumo wa kujiajiri na kama wataajiriwa, basi wawe wapo vizuri,” Profesa Sedoyeka alifafanua.

Msomi huyo pia alisema wameanzisha astashahada na stashahada ya usimamizi wa biashara na lugha ya Kichina kwa lengo la kutoa fursa kwa vijana kuingia kwenye biashara ya kuongoza watalii ambayo imeshika kasi katika Jiji la Arusha.

“Kwa sababu Jiji la Arusha ni la utalii, wale waongoza watalii wanalipwa Dola za Marekani 30 kwa siku, lakini wale wanaofahamu lugha ya Kichina wanalipwa Dola za Marekani 300, hii itatoa fursa kwa vijana wetu kujikwamua kiuchumi na kulipa kodi serikalini,” alisema.


## OFISI YA RAIS
## TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
## HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG

SIMU NA :027-2530022
Nukushi Na:027-2530022
Barua pepe:ded@hanangdc.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W),
S.L.P. 2,
KATESH-HANANG,
MANYARA.
12/08/2020

**TANGAZO LA KUKODISHA SHAMBA LA GAWAL NA BASSOTU.**

**ZABUNI NA. LGA/059/2020-2021/NC/08**

Halmashauri ya Wilaya ya Hanang inawatangazia wananchi wote, watu binafsi na Makampuni kuomba Zabuni ya ukodishaji wa mashamba ya Halmashauri yaliyopo eneo la Gawal lenye ukubwa wa ekari mia sita arobaini na tisa (649) na Bassotu lenye ukubwa wa ekari elfu tisa (9000). Mashamba yako kwenye maeneo mazuri yenye udongo wenye rutuba.

**MASHARTI YA ZABUNI**

1. Mwombaji wa Zabuni anatakiwa kulipa ada ya maombi ya Zabuni kiasi cha Tshs 50,000/= benki ya NMB baada ya kupewa Bill na Mhasibu wa Mapato Halmashauri ambayo haitarudishwa.
2. Mwombaji wa Zabuni atapewa nyaraka za Zabuni “Tender Document” na Katibu wa Bodi ya Zabuni siku za kazi kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa saa 1:30 asubuhi hadi saa 9:30 alasiri kuanzia tarehe 12/08/2020 hadi tarehe 31/08/2020 katika Ofisi namba 18(ofisi ya manunuzi).Hivyo kwa mujibu wa kanuni ya 13(5) na 187(4-5) G.N.446 ya 2013 tumeongeza muda wa ufunguzi wa zabuni hadi tarehe 18/9/2020.
3. Mwombaji atakayeshinda Zabuni ataingia Mkataba wa msimu moja tu baada ya kulipia ekari alizoomba,kuanzia Septemba 2020 hadi Juni 2021 na haruhusiwi kupanda mazao ambayo ukomavu/uvunaji wake utavuka msimu mwingine.
4. Mwombaji atakayeshinda Zabuni atatakiwa kulitumia shamba hilo kwa shughuli za kilimo tu na siyo shughuli nyingine kama vile ufugaji au uchungaji wa mifugo na ikiwa atafanya shughuli ambazo sio za kilimo Halmashauri itamnyang’anya shamba hilo bila kurejeshewa au kurudishiwa fedha za ukodishaji.
5. Ikiwa Mzabuni hatavuna mazao kutokana na hali ya hewa yaani ukame, mafuriko au wadudu waharibifu na mambo mengine ambayo yanafanana na haya, Halmashauri haitahusika na hasara hiyo.
6. Mzabuni anatakiwa kupanda mazao ambayo hayaleti uharibifu wa mazingira kulingana na Sheria inayotawala Mazingira.
7. Halmashauri haitahusika na hasara itakayojitokeza katika kulima shamba atakalokodishiwa Mzabuni mfano:- ulinzi wa shamba, uharibifu unaotokana na mifugo na mengine yanayofanana na hayo maana yake ni kwamba majukumu yote yanahusu shamba atakalokodishiwa ni juu ya Mzabuni kuanzia Septemba 2020 hadi Juni 2021
8. **Mzabuni anatakiwa kutaja bei ya kukodisha shamba kwa ekari moja.**
9. Mzabuni ataje aina ya mazao anayohitaji kupanda katika eneo/shamba analoomba.
10. Mzabuni anatakiwa kutoharibu makinga maji **“Contours”** ambayo yapo katika shamba kwa kuyalima au kuyaondoa.
11. Mzabuni atatakiwa kulipa fedha zote za ukodishaji wa shamba ndani ya siku kumi na nne (14) baada ya kupewa barua ya kukubaliwa na ataingia mkataba na kupimiwa ekari alizolipia na kuoneshwa eneo lake ndani ya siku saba (7) baada ya kulipia.
12. Kama kutatokea kutoeleweka au kutoelewana katika utekelezaji wa sharti lolote la Mkataba utakaofungwa kati ya Halmashauri na mshindi wa Zabuni (Mkulima) pande zote mbili zitakaa na kutatua tatizo kwa njia ya majadiliano. Ikiwa majadiliano yatashindwa kuleta muafaka suala hilo litapelekwa kwa msuluhishi ambaye ni Meneja wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) tawi la Katesh na ikiwa usuluhishi utashindikana shauri la suala hilo litapelekwa Mahakamani.
13. Mwombaji wa Zabuni anaweza kupewa idadi ya ekari alizoomba au kupewa pungufu kwa kutegemea idadi ya waombaji.

**Barua zote za maombi ziandikwe kwa anuani ifuatayo:**
**KATIBU WA BODI YA ZABUNI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG,**
**S.L.P 2,**
**KATESH – HANANG**

Juu ya bahasha iandikwe **Zabuni ya ukodishaji shamba la Halmashauri lililoko Gawal au Bassotu.**

1. Mwisho wa kuleta maombi na kupokea maombi ya Zabuni ni siku ya jumatatu tarehe 31/09/2020 saa 5:00 asubuhi kwenye ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Hanang. Hivyo kwa mujibu wa kanuni ya 13(5) na 187(4-5) G.N.446 ya 2013 tumeongeza muda wa ufunguzi wa zabuni hadi tarehe 18/9/2020 saa tano kamili asubuh.
2. Maombi ya zabuni ambayo hayataletwa na kupokelewa na kusomwa siku ya ufunguzi hayatakubalika.

**GEOFREY ABAYO**
**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)**
**HANANG**

215884002




Mfamasia wa Hospitali ya Wilaya ya Rufiji, Nickolas Slinder (kushoto), akimhudumia muumini wa kiislamu wa dhehebu la Shia Ithna-shariya, Hussein Ramadhani, mkazi wa Ikwiriri, wakati wa uchangiaji wa damu, ulioratibiwa na The Bilal Muslim Mission of Tanzania tawi la Ikwiriri, Rufiji mkoani Pwani, juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# TBS yatakiwa kuandaa kanzidata kwa bidhaa zilizo chini ya viwango

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imelitaka Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kupitia ofisi zake za Kanda ya Ziwa, kuandaa kanzidata ya bidhaa zote zinazoshiriki Maonyesho ya Biashara Afrika Mashariki 2020 ambazo hazina alama ya ubora, kuchukua sampuli zake na kumpatia taarifa.

Hayo yalisemwa jana jijini Mwanza na Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara, Prof. Riziki Shemdoe, kupitia hotuba yake aliyoitoa kwenye maonyesho hayo ambayo yameandaliwa na Chemba ya Biashara, Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIAO yakifanyika viwanja vya Rock City Mall.

"Naomba nipatiwe taarifa ya suala hilo kabla ya mwisho wa mwezi huu," alisisitiza Prof. Shemdoe wakati wa ufunguzi wa maonyesho hayo. Katibu Tawala Mkoa wa Mwanza, Emmanuel Tutuba, alishauri TBS kuendelea kutoa elimu kwa wajasiriamali wadogo kwa kuwafuata walipo kuliko kusubiri mpaka wawafuate maofisini.

Kaimu Mkuu wa Kanda wa TBS, Evarist Mrema, alisema TBS ni moja ya wadau wakubwa katika maonyesho hayo ikizingatiwa kuwa kiwango ni suala muhimu katika ukuaji wa viwanda, kwa kuwa uzalishaji wa bidhaa zenye viwango unawaongezea imani wanunuzi na kuwawezesha wenye viwanda kuwa na ushindani sawia na kupata masoko ndani na nje ya Tanzania.

"Vilevile tunawahamasisha wafanyabiashara wenye majengo ya hoteli, migahawa, maghala, maduka ya vipodozi na chakula na 'supermarket' kufika katika maonyesho haya kupata huduma ya kusajili majengo yao hapa hapa.

Cha muhimu waje na nakala ya TIN na leseni ya biashara," alisema Mrema.

Mrema alibainisha kuwa hadi sasa TBS Kanda ya Ziwa imeshapokea zaidi ya maombi 2,000 ya kusajili majengo ya chakula na vipodozi.

Naye Ofisa Masoko Mwandamizi wa TBS, Gladness Kaseka, alisisitiza kuwa ni muhimu kwa wafanyabiashara na wazalishaji kuzingatia taratibu zilizowekwa kwani kwa kufanya usajili na kuthibitisha bidhaa zao wataepuka hasara kwa biashara zao kufungiwa au wakati mwingine kulipa fidia zitokanazo na adhabu za ukiukwaji wa Sheria ya Viwango Na. 2 ya mwaka 2009.

"Huduma hii kwa kawaida inapatikana kupitia mfumo wa kimtandao (OAS) unaopatikana kupitia tovuti ya TBS (www.tbs.go.tz) ambapo mteja itampasa kujisajili mwenyewe kupitia mfumo," alisema Kaseke na kuongeza;

"TBS kwa mara ya kwanza ilianza kutoa huduma hiyo katika maonyesho ya 8'8 ili kuwasaidia wateja ambao wanakutana na changamoto katika kujisajili wanafanikisha usajili wao na kuepuka usumbufu wa kufanya biashara isiyo rasmi."

# Watumishi wanolewa kuongeza weledi, ufanisi

**Na Mwandishi Wetu**

WATUMISHI wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (OR-MUUUB), wapatiwa mafunzo yatakayowawezesha kufanya kazi kwa kuzingatia weledi na ufanisi ili kuboresha utoaji huduma kwa umma na wadau wengine.

Hayo yalisemwa jana na Kaimu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Dk. Francis Michael, wakati akifungua mafunzo ya siku tatu kwa watumishi wa ofisi yake yatakayotoa fursa ya kuwajengea uwezo kwenye eneo la uandishi wa nyaraka za ofisi, utunzaji bora wa kumbukumbu na nyaraka, mapambano dhidi ya rushwa ikiwamo namna bora ya kukabiliana na msongo wa mawazo mahala pa kazi.

Dk. Michael aliwaka watumishi hao kufuatilia kwa umakini mafunzo hayo ili wapate elimu na weledi kuhusu namna bora ya uandishi wa nyaraka, utunzaji wa kumbukumbu na nyaraka, kuepuka vitendo vya rushwa na msongo wa mawazo ambavyo kwa kiasi kikubwa vinaweza kuathiri utendaji kazi wao wa kila siku.

"Mafunzo haya ni muhimu katika kuiwezesha ofisi kupata watumishi mahiri, waadilifu, wenye kuzingatia weledi na ufanisi kiutendaji," alisisitiza

Dk. Michael. Dk. Michael alifafanua kuwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kama zilivyo taasisi nyingine nyeti, inapaswa kuwa na watumishi bora na wenye ujuzi na maarifa yatakayowaongezea ufanisi kiutendaji na ndio maana menejimenti imeamua kuwapatia mafunzo yatakayowajengea uwezo wa kutoa huduma bora kwa wananchi na wadau wengine.

Mafunzo hayo yanayofanyika katika Chuo Kikuu cha Dodoma, yalianza jana na yatamalizika kesho na yanawashirikisha watumishi 218.

# Kaya 6,174 zaenguliwa mpango wa umaskini

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

JUMLA ya kaya 6,174 katika mkoa wa Kagera zimeondolewa katika orodha ya wanufaika wa mpango wa kunusuru kaya maskini TASAF awamu ya tatu, baada ya kukosa sifa.

Akizungumza na Nipashe, Mratibu wa TASAF Mkoa wa Kagera, Ephraz Mukama, alisema wakati mpango huo unaanza walianza na kaya 68,915 na sasa zimesalia kaya 62,741.

Mukama alisema sababu kubwa za watu hao kuondolewa katika orodha ya wanufaika ni baadhi kufariki, kuhama na wengine kubainika kuingizwa katika mpango kinyume na utaratibu.

Aidha, alisema mbali na kaya hizo kuondolewa sasa wameanza zoezi la kuingiza kaya mpya zenye uhitaji ambazo hazikuwamo katika awamu zilizotangulia.

"Wananchi wafike katika ofisi za vijiji na mitaa na kuhudhuria mikutano ya hadhara ya kuibua kaya maskini, ili zenye sifa ziorodheshwe, maana tayari wenyeviti wa vijiji na mitaa wamekwishapewa maelekezo," alisema.

Alisema Rais John Magufuli alizindua awamu nyingine ya TASAF Februari mwaka huu, na kuwa wakati akizindua alisema mpango huo utawafikia wananchi wote maskini ambao wana kipato cha chini na kufikia vijiji vyote ambavyo vilikuwa vimebaki.

"Fursa hiyo imekwishajitokeza na tumekwishaagizwa kupita katika vijiji vyote na mitaa kuandikisha kaya mpya, wafike katika ofisi za vijiji na mitaa kuuliza utaratibu wa kuandikishwa, lakini itakapoitishwa mikutano ya kuibua wenye sifa wahudhurie," alisema.

Alitaja baadhi ya sifa za kaya duni zinazolengwa kuwa ni zisizoweza kupata milo mitatu kwa siku, zenye watoto wengi na hazina uwezo wa kuwapeleka shule, au hazina uwezo wa kuwapatia huduma za afya.

Mmoja wa wanufaika wa mpango huo, Lydia Anthon, mkazi wa Buyekera katika Manispaa ya Bukoba, alisema kwa mwaka huu amepewa malipo mara moja na kuiomba serikali kuwapatia fedha hizo kwa wakati ili kuwapunguzia makali ya maisha.

"Fedha za TASAF zimekuwa zikitusaidia, lakini sasa tuna muda hatujapewa, tunaomba serikali iendelee kutusaidia maana maisha ni magumu," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Mtaa wa Buyekera Asili, Justinian Kamugisha, alisema mpango huo ni muhimu maana unawasaidia wananchi maskini kupunguza makali ya maisha, lakini akaiomba serikali kuwajengea zahanati katika mtaa wake na kuboresha mazingira ya shule za serikali ambazo ndiyo mkombozi wa watoto wanaotoka katika kaya maskini.

Kwa mujibu wa mratibu wa TASAF, katika kipindi cha mwaka jana, serikali ilitumia zaidi ya shilingi bilioni 2 kuwalipa wanufaika wa mpango huo Kagera.



Mafundi wa kampuni ya Nyanza Road, wakiwa katika ujenzi wa mifereji ya maji ya mvua katika barabara ya Kitunda, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wazazi wanavyochangia watoto kufeli shuleni

**Na Christina Haule,**
MOROGORO

UPUNGUFU (ikama) wa walimu katika shule za msingi zilizopo maeneo ya vijijini nchini unaweza kuisha ikiwa wazazi watakuwa tayari kuwasaidia watoto wao kimasomo ili wafaulu vizuri darasa la saba na kujiendeleza.

Tatizo hilo linaweza kupata ufumbuzi kutokana na mpango wa serikali uliopo wa kupeleka walimu kulingana na mkoa walipotoka.

Ofisa elimu anayeshughulika vifaa na takwimu msingi, Agnes Mhamilawa Wilaya ya Morogoro, alisema hayo wakati akijibu hoja za viongozi wa vituo vya taarifa na maarifa vilivyoandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP –Mtandao) kutoka kwenye kata mbalimbali wilayani humo waliopitia bajeti ya mwaka 20/21 kwa mrengo wa kijinsia na kuona upungufu wa walimu katika wilaya hiyo ambao umekuwa haufanyiwi kazi mwaka hadi mwaka.

Mhamilawa alisema Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro ndio inaongoza katika halmashauri zote nchini kuwaambia watoto wao wasifanye vizuri katika mtihani wa darasa la saba, ili wafeli kwa visingizio kuwa hawana uwezo wa kuwasomesha.

Alisema kisingizio hicho na vingine ya kuwakatisha tamaa watoto kuendelea na elimu vimekuwa vikiongezeka, hivyo kuchangia kutokuwapo walimu wa kutosha katika shule nyingi, na kwamba mpaka sasa kuna shule 45 za msingi zenye walimu chini ya wanne.

"Kuna shule ina walimu watatu, huku wanafunzi wakiwa 1,043, muhimu tuombe Mungu serikali iajiri walimu kwa sababu hata tukitaka kurekebisha kwa kuongeza idadi ya walimu, tutaanzia na hizo shule 45," alisema. Hivyo aliwaomba wahamasishaji hao kutoka TGNP kuendelea kutoa elimu kwa njia mbalimbali ikiwamo maigizo ya kuwafanya wazazi kuona umuhimu wa kusomesha watoto wao.

Mhamilawa alisema, changamoto ya jiografia ya wilaya hiyo pia huchangia upungufu wa walimu, kufuatia walimu wengi kutoka mikoa mbalimbali huleta barua za kuhamishwa kutoka makao makuu, hivyo shule hizo kuendelea kukosa walimu.

Akizungumzia bajeti hiyo kutotengewa fedha kwa ajili ya taulo za kike, matundu ya vyoo, chumba rafiki kwa mtoto wa kike, madarasa na maboma ya nyumba za walimu Mhamilawa alisema fedha hizo haziingii kwenye bajeti bali wao huziomba kama bakaa na tayari wameshapokea Sh. milioni 282 kutoka serikalini, huku wakipokea Sh. milioni 200 kutoka kwa wadau wa elimu, na wanatarajia kupokea Sh. milioni 250 kwa ajili ya kutekeleza mahitaji hayo. Naye Mwenyekiti wa kituo cha Taarifa na maarifa Kata ya Mkambarani, Teresia Berege, aliishukuru halmashauri hiyo kwa sasa kutambua bajeti ya mrengo wa kijinsia na kuizungumzia vizuri tofauti na zamani ambapo walipozungumzia taulo za kike, wanaume walikuwa wakiziba midomo na kushindwa kuongelea.

Mwakilishi wa Ofisa Elimu ya Sekondari, Miraji Saidi, alisema tayari kiasi cha Sh. milioni 50 kimetengwa kwa ajili ya taulo za kike kwenye shule za sekondari wilayani humo.

# Morogoro kujengewa mradi mkubwa wa maji

**Na Frank Kaundula,**
MOROGORO

KATIKA kuhakikisha wananchi wa Mkoa wa Morogoro wanaondokana na tatizo la maji, Kampuni ya DON Cosult pamoja na ya CDM SMITH ya nchini Ujerumani zimedhamiria kujenga mradi mkubwa ili kuboresha huduma ya maji kwa jamii.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (MUROWASA), Mhandisi Tamimu Katakweba, alisema kuwa mradi huo wa miaka mitano utakagharimu Sh. bilioni 180.

"Baadhi ya maeneo yanakabiliwa na uhaba wa majisafi na salama hivyo napenda kuchukua nafasi hii kutamka kuwa sasa changamoto hiyo inakwenda kupotea kwa kuwa kuna mradi mkubwa unatengwa," alisema Katakweba.

Alisema walikutana kampuni ya DON Cosult na CDM SMITH ya nchini Ujerumani kwa lengo la kutaka kuangalia utekelezaji wa mradi huo wa uboreshaji huduma ya maji katika mkoa huo.

Katika makubaliano hayo Mhandisi Katakweba alisema kuwa mradi huo wa miaka mitano utakaogharimu Euro milioni 70 sawa na Sh. bilioni 180 za kitanzania ulisainiwa jijini Dodoma na utaanza kutekelezwa mwishoni mwa mwaka huu.

Alisema baada ya kukamilika wananchi watapata majisafi na salama kwa uhakika na hayo yote yanatokana na jitihada za serikali za kutatua kero mbalimbali za wananchi hususani wanyonge nchini.

Aliwataka wananchi kuendelea kuwa na subira katika kipindi hiki na baada ya hapo huduma ya maji itapatikana saa 24 hususani maeneo ambayo huduma hiyo imekuwa ikipatikana kwa kusuasua kila wakati na kusababisha malalamiko mengi.

Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya Don Cosult, Mangyu Seni, alisema lengo ni kutaka kuboresha huduma ya upatikanaji wa maji kwa mji wote wa Morogoro, hivyo uwapo wa mradi huo utasaidia kuimarisha huduma hiyo.

"Ni kweli kuwa kumekuwa na malalamiko ya wananchi juu ya kukosekana kwa huduma ya maji ya uhakika kwa baadhi ya maeneo hivyo baada ya mradi huu kukamilika malalamiko hayo kamwe hayatasikika tena hapa," alisema Seni.

Wananchi wa mkoa huo wameipongeza serikali kwa kitendo cha kuboresha huduma hiyo muhimu ya maji kwa jamii na kwamba uwepo wa mradi huo kutaondoa uhaba wa maji maeneo mengi ya Morogoro.

# RC Ndikilo awabana waliofeli madawati

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Evarist Ndikilo, amewataka wakuu wa wilaya za mkoa huo ambao hawajatekeleza agizo la kutengeneza madawati kumpa maelezo ya sababu zilizowakwamisha.

Akiongea wakati alikabidhiwa madawati na Mkuu wa Wilaya ya Rufiji, Luteni Kanali Patrick Sawala mjini Kibaha, Ndikilo alisema agizo hilo alilitoa mwezi mmoja uliopita lengo likiwa ni kumaliza tatizo la watoto kukaa chini katika mkoa huo.

"Wakuu wa wilaya ambao hawajakamilisha kutengeneza madawati nipate maelezo ya kina yenye sababu za mashiko tujue kwanini hawajakamilisha hadi sasa," alisema Ndikilo.

Alisema, mkoa huo umejipanga kuhakikisha hakuna mwanafunzi anayekaa chini, ili wanafunzi wapate elimu katika mazingira bora.

"Tulikubaliana na wakuu wa wilaya katika kikao kazi tulichoketi mwezi mmoja uliopita hatuwezi kuwa na watoto wanaokaa chini na tarehe moja leo ndio ilikuwa mwisho," alisema.

Alisema, uwapo wa madawati ya kutosha shuleni utamsaidia mwanafunzi kuacha utoro, na mwalimu atakuwa anafundisha katika mazingira mazuri.

Aliwahimiza wakurugenzi kuacha kukimbilia kutengeneza madawati, viti na meza kwa bei rahisi badala yake waende sehemu zenye matengenezo yenye ubora.

"Madawati haya yanayotengenezwa hapa katika Shirika la Nyumbu ni tofauti na mitaani, yana uwezo wa kudumu kwa miaka mitano, tofauti na huko mtakakoenda ambako kila mwaka mtakuwa mnatenga bajeti kukarabati au kutengeneza upya," alisema.

Katibu Tawala Mkoa wa Pwani, Dk. Delphine Magere, alimpongeza Mkuu wa Wilaya ya Rufiji kwa kutekeleza agizo la Mkuu wa Mkoa kwa wakati.

Alisema kaulimbiu ya Pwani, 'Hakuna kukaa chini' itatekelezwa kwa vitendo kwa kuwa mkoa huo ni wapiganaji wanaopigania nchi na kwa hivyo nchi itakuwa na wasomi wa kupeleka uchumi mbele.

Akikabidhi madawati hayo kwa Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya ya Rufiji, Luteni Kanali Patrick Sawala, alisema, wilaya hiyo ilikua na upungufu ya meza 1,882, viti 231 na madawati 3,945 na wamejipanga kuhakikisha wanatekeleza mpango huo.

Alimshukuru Mkurugenzi wa Shirika la TACT Nyumbu, kwa kumaliza matengenezo ya viti na meza 300 kwa wakati.

Mkurugenzi wa Shirika la TACT Nyumbu, Brigedia Jenerali Hashimu Komba, alisema mwitikio ni mkubwa kwa watendaji kuitikia agizo la Mkuu wa Mkoa kutumia shirika hilo kutengeneza madawati, viti na meza zinazohitajika.

Alisema, pia wanatarajia kukabidhi viti na meza 400 kwa ajili ya Wilaya ya Mkuranga.

# Tiba mbadala walia ukubwa wa gharama

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAGANGA wa tiba asili na tiba mbadala nchini, wamelalamikia gharama kubwa zinazotozwa na serikali kwa ajili ya kusajili dawa zao.

Wamesema gharama hizo ni kubwa sana, hali inayosababisha wengi wao kushindwa kuzimudu.

Hayo yalielezwa jana na waganga hao, katika maadhimisho ya siku nne ya tiba asili ya Mwafrika yanayoendelea jijini Dodoma.

Bashiru Iddy, mwakilishi wa Shekilindi Bosnia ant-covid, watengenezaji wa moja ya dawa ambayo ilitumika katika mapambano dhidi ya virusi vya corona mwaka huu, alisema wanaiomba serikali kupunguza gharama hizo.

Iddy alisema kuwa hivi sasa gharama za usajili wa dawa zimekuwa kikwazo kikubwa kwa waganga, hali ambayo inasababisha wengi wao kuuza bila kusajiliwa.

Naye Mwenyekiti wa Waganga Kata ya Nkinga Wilaya ya Igunga Mkoa wa Tabora, Ishila Intenya, alisema pamoja na gharama za usajili wa dawa kuwa juu, lakini wamekuwa wakizungushwa kwa muda mrefu.

# Asasi yaasa matumizi mabaya ya mitandao

**Na Elizabeth Zaya**

SHIRIKA la Mtandao Tanzania (Internet Society), limetoa wito kwa jamii kuepukana na taarifa za uongo, hususani katika kipindi hiki cha uchaguzi mkuu ili kutokusababisha taharuki.

Kauli hiyo ilitolewa jijini Dar es Salaam na Rais wa taasisi hiyo Kanda ya Tanzania, Nazzar Nicholas.

"Taarifa za uongo zinasababisha msongo na taharuki kwa mtu na jamii na wakati mwingine husababisha vifo. Katika kipindi hiki cha uchaguzi ni hatari sana kwa mstakabali wa umoja wetu kama Watanzania," alisema Nicholas.

Alisema ni vema kuhakiki taarifa yoyote ambayo mtu anaipata kabla ya kuisambaza kwa wengine.

"Ni vizuri kabla ya kurusha au kusambaza taarifa yoyote uihakiki kwanza ili usisababishe taharuki," alisema Nichoplas.

Pia aliwashauri wote wanaotumia mitandao ya kijamii kuwa makini na matumizi ya akaunti zao katika kipindi hiki cha uchaguzi.

"Tunashauri kwamba kila mwenye akaunti ya kijamii kujenga tabia ya kubadili 'password' mara kwa mara kwa kuweka mchanganyiko wa herufi ambazo itakuwa si rahisi kwa matapeli pamoja na wale wenye nia ovu za kisiasa mitandaoni kudukua," alisema Nicholas.

# Ubovu barabara wapaisha gharama usafirishaji mazao

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKAZI wa Halmashauri ya Msalala wamesema ubovu wa barabara inayounganisha Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga na Mkoa wa Geita, imesababisha ongezeko la gharama za usafirishaji wa dengu.

Gharama zilizoongezeka ni za usafirishaji kutoka shambani hadi sokoni kwa shilingi 50,000 kwa gunia moja la dengu la debe saba. Ongezeko la bei hiyo linaongezeka kila msimu wa kilimo kutokana na wamiliki wa magari makubwa ya kubeba mizigo, kulalamika kuwa magari yao yanaharibika kutokana na ubovu wa barabara. Awali walikuwa wakisafirisha kwa shilingi 30,000 kwa gunia moja.

Barabara hiyo inaurefu wa kilometa 107 kutoka wilayani Kahama kupitia Halmashauri ya Msalala, Bukori hadi mkoani Geita. Hata hivyo, serikali iliahidi kuwa imetengewa shilingi bilioni 70 kutengenezwa kwa kiwango cha lami.

Waliyabainisha jana wakati mgombea ubunge wa Jimbo la Msalala CCM Iddi Kassimu Iddi, alipokuwa katika ziara ya siku moja ya kujitambulisha kwa wananchi baada ya kumshinda kwenye kura za maoni aliyekuwa mbunge wa jimbo hilo, Ezekiel Maige. Kevin Bakari, Mkazi wa Kata ya Segese, alisema kuwa katika Halmashauri ya Msalala Kata ya Segese inaongoza kwa kilimo cha dengu, mpunga, mahindi na choroko, lakini bei ya usafirishaji wa dengu hadi sokoni ni gharama kubwa kulinganisha na mazao mengine ya biashara. Alisema gunia moja la dengu linasafirishwa kwa shilingi 50,000 hadi sokoni, huku mpungu ukisafirishwa kwa shilingi 1,000 hadi 2,000 kwa gunia moja na ongezeko hilo linatokana na ubovu wa barabara inayounganisha Wilaya ya Kahama, Bukori hadi Geita.

Naye Angelina James, alisema wamekuwa wakipata hasara wakati wakisafirisha matunda hasa matikitiki maji, yanafika sokoni yakiwa mengi yameboneyea na mwisho wa siku wanayauza kwa bei ndogo ukilinganisha na gharama walizotumia wakati wa maandalizi ya shambani.

Pendo Edward, alimtaka mgombea wa jimbo hilo, Iddi Kassim endapo atapatiwa ridhaa ya kuwaongoza, ahakikishe anasimamia ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami ili kupuguza gharama za usafirishaji wa mazao ya kibiashara.

Ajikibu hoja hizo, Kassimu Iddi alisema, moja ya kipaumbele chake ni kuhakikisha barabara hiyo inajengwa kwa kiwango cha lami kama ilivyoelezwa kwenye ilani ya uchaguzi, ili kufungua fursa za kibiashara kwa kusafirisha mazao ya biashara hadi sokoni kwa bei nafuu.




Mkuu wa Kitengo cha Biashara Halopesa, Magesa Wandwi (kulia), akibadilishana hati za makubaliano na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Umoja Switch, Danford Mbilinyi baada ya kusaini makubaliano jijini Dar es Salaam jana, ambapo wateja wa Halopesa wataweza kutoa fedha kwenye ATM za Umoja Switch. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# HaloPesa, UmojaSwitch wazindua huduma ya ATM

**Na Mwandishi Wetu**

HALOTEL kupitia huduma yake ya HaloPesa, imeingia ubia na Kampuni ya UmojaSwitch kwa wateja wa HaloPesa ya kutoa fedha kupitia ATM za Umoja zilizoko nchini.

Hatua hiyo inatokana na kasi ya ukuaji wa teknolojia na uchumi, Halopesa imeendelea kutanua wigo wa kutoa huduma zake za kifedha nchini katika mkakati wa kitaifa wa ujumuishwaji wananchi katika matumizi ya mifumo rasmi ya kifedha chini.

Akizungumza katika uzinduzi wa huduma hiyo katika ofisi za Makao Makuu ya Halotel, Mkuu wa Kitengo cha Biashara wa Halopesa, Magesa Wandwi, alisema ni hamasa na lengo la kampuni hiyo kuhakikisha wanaendelea kutumia miundombinu ya teknolojia na fursa zote zilizopo kwa kushirikiana na wadau mbalimbali katika sekta ya huduma za kifedha na kuwapa wateja wao huduma bora na za uhakika.

"Nifuraha yetu leo kushirikiana na UmojaSwitch kuzindua rasmi huduma hii ambayo itawawezesha wateja wa Halopesa kutoa fedha kwa urahisi na uhakika zaidi kupitia ATM za Umoja zaidi ya 250 zilizopo maeneo mbalimbali kote nchini," alisema. Wandwi alisema huduma hiyo haitakuwa na makato ya ziada tofauti na makato ya kawaida ya kutoa pesa kwa wakala wa kawaida, pia huduma hiyo haitahusisha matumizi ya intaneti pale mteja atakapokuwa anatoa fedha kwenye ATM za Umoja.

Pia, mawakala wa Halopesa zaidi ya 50,000 waliosambaa nchini kwa pamoja wataendelea kuwahudumia wateja wa Halopesa zaidi ya 2,000,000 waliopo mijini na vijijini.

"Mteja wa Halopesa atapitia hatua za kawaida kutoa pesa kwa kupiga *150*88# kisha kuchagua '2', (Kutoa Pesa), kisha chagua tena "2" (UmojaATM), ataendelea na kuweka kiasi na namba yake ya siri ya Halopesa, baada ya hapo atapata ujumbe wenye namba ya siri ya uthibitisho ambayo ataitumia kutoa fedha katika ATM za Umoja, aliongeza Magesa.

Akiongea na waandishi wa habari katika uzinduzi huo, Mkurugenzi Mkuu wa UmojaSwitch, Danford Mbilinyi, alisema ushirikiano na Halopesa utaongeza upatikanaji wa huduma za kifedha kirahisi nchini kupitia ATM zaidi ya 250 zilizoenea nchi nzima na kwamba wateja wa HaloPesa wana fursa nyingine ya uhakika sasa ya kupata fedha muda wowote mahali popote nchini.

ama

ALHAMISI SEPTEMBA 3, 2020

AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12

**Taasisi zilikumbuka kuwakinga wenye uhitaji maalum corona?**




Ukurasa 14

Mabadiliko haya yanavyotishia hatima ya maskini hasa Afrika



Ukurasa 14

**'Kuzaliwa bila 'jinsi' hakunitishi'**

MAZINGIRA

# Ni janga barakoa

• Kitisho afya wenye walemavu, watoto • Chanzo kusambaza maradhi

**Na Sabato Kasika**

MWAKA 2020 umetikisa dunia kimaradhi kutokana na kuzuka kwa ugonjwa wa COVID-19, unaoambukizwa kwa njia ya hewa, hivyo kulazimisha uvaaji wa barakoa .

Licha ya kwamba kwa Tanzania ugonjwa huo umedhibitiwa kabla haujaleta madhara makubwa, kama mataifa mengine serikali ilihimiza uvaaji wa barakoa, kunawa mikono, kutumia vitakasa mikono na kujiweka mbali na misongamano kama njia ya kujikinga.

Uvaaji wa barakoa ulienea zaidi kwenye majiji makubwa kama Dar es Salaam, Arusha, Mwanza na Dodoma.

Lakini, pamoja na juhudi hizo, inaelezwa na Mtaalam Mshauri wa Mazingira kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais, Dk. Hussein Omar, kuwa taifa linahitaji kuandaa namna bora ya kuteketeza taka za barakoa.

"Kuna ukiukwaji Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Mazingira ya mwaka 2004 kuhusu utupaji taka zikiwamo barakoa, tukirejea kifungu cha 137." Anaeleza Dk. Omar kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais.

Kifungu 137 kwa mujibu wa maelezo yake kinaagiza yafuatayo-137mosi, Waziri, kwa kushauriana na Waziri mwenye dhamana ya masuala ya afya, atahakikisha kwamba taka zitokanazo na huduma za afya zinachambuliwa na kutunzwa katika kontena maalumu zilizobainishwa na kusafirishwa kwenye magari maalumu yaliyoundwa na kusajiriwa kwa madhumuni hayo.

Katika kifungu cha (2) kinasisitiza kuwa Waziri, kwa kushauriana na Waziri mwenye dhamana ya masuala ya afya, ataagiza njia bora zaidi ziwezekanazo kwa ajili ya utupaji wa mwisho wa taka za aina mbalimbali zinazozalishwa kutokana na huduma za afya.

Kadhalika katika kifungu cha (3) kinasema "taka zitokanazo na huduma za afya;" zinajumuisha, lakini hazitahusisha tu taka zenye kuambukiza magonjwa, taka za kipatholojia, vitu vyenye ncha kali, dawa, genetoksiki, taka zenye mionzi, taka za mgando wa damu na dawa za binadamu.

Katika mahojiano na gazeti hili jijini Dar es Salaam hivi karibuni, Dk Omar anasema, hakuna utaratibu rasmi uliowekwa katika jamii wa kuhakikisha barakoa ambazo zimeshatumika zinakusanywa, kuhifadhiwa na kuteketekezwa, kwa mujibu wa sheria.

Dokta Omar anasema, badala yake zinatupwa ovyo hali hiyo inaiweka jamii hasa watoto, walemavu wa akili, vijana na kinamama wanaojihusisha na uzoaji wa taka wapo katika hatari ya kupata magojwa.

"Mamlaka hazijaweka mipango maalum wa ukusanyaji, uhifadhi na uteketezaji wa barakoa zilizokwishatumika, badala yake zinatupwa ovyo. Hali hiyo inaweza kuiweka jamii za makundi hayo katika hatari ya kupata magojwa mbalimbali," Dk. Omar anasema.

Mtaalam huyo mshauri anataja baadhi ya magonjwa ambayo yanaweza kusababishwa na hali hiyo ya utupaji wa barakoa kuwa ni corona na kifua kikuu (TB) na kuwataka Watanzania kuepuka mtindo huo.

Anasema, hakuna utaratibu rasmi uliowekwa katika jamii kuhakikisha barakoa zilizokwishatumika zinakusanywa, kuhifadhiwa na kuteketekezwa kwa kuzingatia matakwa ya sheria.



Barakoa zikiwa zimetupwa baada ya kutumika. **PICHA: MTANDAO**

"Sasa ni wakati muafaka kwa serikali za mitaa nchini kwa kushirikiana na wadau wengine kuweka mpango maalum wa kuelimisha jamii namna ya kudhibiti barakoa zilizokwishatumika," anasema.

Anasema, hatua hiyo inaweza kuhusisha jamii kuziharibu barakoa baada ya kuzitumia, kutumia vyombo vya kuhifadhia taka katika maduka ya dawa ama kuwaelimisha watoa huduma za uzoaji taka kuzitenganisha barakoa wakati wa kuzikusanya na kuzipeleka kwenye hospitali za serikali kwa ajili ya uteketezaji.

"Matumaini yangu ni kwamba, mikakati hii na mingine ambayo inaweza kutolewa na wataalam wa afya itaweza kupunguza kama si kuondoa hatari ya maambukizi ya magonjwa mbalimbali kwa jamii," anasema.

**MAENEO HATARI**

Kwa upande wake Dk. Phoibe Koshuma, anasema, suala la usafi wa mazingira lina upana wake, kwa vile linaanzia nyumbani hadi mitaani, hivyo ni muhimu kila mtu kulizingatia, ili kuepuka kuambukizwa maradhi bila kujua.

Dk. Koshuma, ambaye ni mstaafu kutoka Kituo cha Afya Sinza Dar es Salaam, anasema, usafi wa mazingira ni njia ya kuendeleza afya kwa kuzuia mawasiliano ya binadamu na athari za taka, kwa kuwa athari hizo zinaweza kuhusu mwili, mikrobiolojia, biolojia au kemikali vikolezo vya ugonjwa.

"Taka ambazo zinaweza kusababisha matatizo ya afya ni taka za hospitalini, za vyooni hasa kinyesi cha binadamu na cha wanyama, takataka ngumu, za viwandani, majitaka, za kilimo na kwamba zote hizo hazitakiwi kuzagaa,"Dk Koshuma anasema.

Anaongeza kuwa usafi ni njia kuu ya kuzuia maradhi na unaweza kutumiwa kwa kutibu majitaka, kuwa na vyoo, kuwa na viteketeza taka na matendo ya usafi binafsi kama kuosha mikono kwa maji safi na sabuni.

"Usafi wa mazingira kama unavyoelezwa na Shirika la Afya Duniani (WHO), unahusu pia kudumisha ratiba ya usafi, kwani uchafu wa mazingira ni sababu kuu ya maradhi duniani," anasema.

**INAENDELEA UK.12**

AFYA

# Taasisi zilikumbuka kuwakinga wenye uhitaji maalum corona?



Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Kongowe,Magige Mwita (katikati), akipokea msaada wa vifaa vya kunawia mikono kutoka kwa Mratibu wa Chama cha Msalaba Mwekundu Mkoa wa Pwani, Everist Mayuya. **PICHA: JASMINE PROTACE**

**Na Yasmine Protace,** KIBAHA

UMUHIMU wa kunawa mikono ni suala lisilokwepeka ni la lazima kwa kuwa ndiyo njia pekee ya kuondoa na kuiepusha jamii na maradhi yakiwamo magonjwa ya mlipuko na zama hizi COVID -19.

Kusafisha mikono kabla ya kushika chakula, kula na baada ya kutumia choo kunaelezwa kuwa kunaepusha maradhi yakiwamo kuhara na kutapika, corona , macho na ngozi, kinasema chama cha Msalaba Mwekundu Tanzania mkoani Pwani.

Lakini, kundi mojawapo lililosahaulika katika kupatiwa vifaa vya kunawa mikono ni wahitaji kama wanaoishi na ulemavu. Hawa wanahitaji vifaa maalumu vya kunawia kuanzia mabomba na masinki maalum kukidhi mahitaji yao.

Chama hicho kinawakumbusha Watanzania kuwa watu wenye ulemavu na wenye uhitaji maalumu wasiponawa kikamilifu mikono wanazoa vimelea vya maradhi na kuvisambaza sehemu nyigine na kuongeza tatizo la kueneza magonjwa.

Ili kuwaepusha wanafunzi na watu wenye uhitaji maalumu na magonjwa ya milipuko, Msalaba Mwekundu Pwani, unakabidhi vifaa vya kujikinga na magonjwa ya milipuko, katika shule za msingi na pia kwa yatima katika wilaya za mkoa huo.

> **Tunampongeza Rais kamtanguliza Mungu wakati wa kupambana na corona na sasa hali inaendelea vizuri na watu wanazidi kufanya shughuli zao za kimaendeleo bila kuhofu.**

Mwenyekiti wa chama hicho, Mkoa wa Pwani, Stephen Sapi, anasema ili kutimiza azma ya kuepusha wananchi wamekabidhi ndoo 100 na mashine 19 kwa ajili ya kunawia mikono katika mkoa huo.

Anashauri msaada wa vifaa hivyo unaopokelewa mkoani hapo upelekwe katika shule za msingi kuhudumia wanafunzi wenye uhitaji maalumu wakiwamo yatima.

Sapi anasema wanazisaidia shule za wilaya ya Kisarawe, Mkuranga, Kibaha Mjini na Vijijini ili kusaidia wanafunzi na kuwafikia wahitaji pia. Anasema: "Pamoja na Red Cross kujishughulisha na masuala ya maafa, kuchangia damu na afya kwa umma, tumeamua kutoa vifaa hivyo ili kuisaidia jamii kujikinga na magonjwa ya milipuko ikiwamo corona."

Anasema jamii ikijua umuhimu wa kunawa mikono, itafanikiwa kutokomeza magonjwa ya milipuko katika maeneo mengi nchini.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mdinhi Kongowe Maige Meita, anasema msaada huo utawafikia na kuwasaidia wanafunzi katika masuala yanayohusu usafi .

Anaeleza kuwa shule yao ina wanafunzi wenye uhitaji maalumu na kwamba watafikiwa na vifaa hivyo.

"Tuna watoto 49 katika shule hii ambao wanaishi na ulemavu. Ndoo za maji ziko mbili na moja inatumiwa na wasichana na nyingine ni kwa ajili ya wavulana,"anasema Meita.

Anaongeza kuwa shule imeweka mabomba ya koki, lakini yanakuwa ni changamoto kwa walemavu kwani hawayafikii hasa wale wenye matatizo ya mikono.

Anasema Msalaba Mwekundu umekuwa msaada mkubwa kwa kuwezesha upatikanaji wa ndoo za maji na sehemu za kuziweka na kwamba ni kubwa zenye ujazo Lita 20 kwa kila moja.

Meita anasema kupatikana kwa msaada wa mashine za maji kutawasaidia wanafunzi walio na ulemavu wa viungo kwani hawatapata shida kutokana na mashine hizo kuwawezesha kufungua na kupata maji.

Pamoja na mwalimu huyo kutoa shukrani kwa kupatiwa ndoo na mashine za maji, anazungumzia changamoto nyingine aliyopo katika shule hiyo akitaja miundombinu kuwa mibovu hali inayowasababishia wanafunzi wenye ulemavu kupata shida ya kutumia kwenye barabara zinazotumiwa na wanafunzi wenye viungo vyote.

"Miundombinu ya shule imeharibika imechimbikachimbika ovyo, walemavu wa miguu wanapata changamoto pale wanapotumia barabara hizo"', anasema Meita na kuomba wadau wengine kuguswa na kumaliza tatizo hilo.

Akipokea msaada huo, Mkuu wa Wilaya ya Kibaha, Martin Ntemo, kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa, anasema kuwa msaada huo utawasaidia wanafunzi katika kujikinga na magonjwa ya milipuko.

Anasema taasisi ya Msalaba Mwekundu imekuwa ikishirikiana na Mkoa wa Pwani katika shughuli za kimaendeleo za kijamii na kiuchumi mara kwa mara.

"Vifaa hivi vitawasaidia wanafunzi kujikinga na magonjwa ya milipuko, pia unawaji wa mikono umeweza kuendelea kudhibiti corona na kuwaweka wanafunzi katika hali ya usalama zaidi,"anasema.

Ntemo anaongeza kuwa, jamii inatakiwa kujikinga na magonjwa ya milipuko kwa kuwa na mazoea ya kunawa mikono mara kwa mara na kuwafundisha watoto kufanya hivyo.

Anazungumzia umuhimu wa kunawa, kuzingatia masharti na kumtanguliza Mungu katika kukabiliana na magonjwa na kusema wanamshukuru Rais John Magufuli kwa kumtanguliza Mungu katika kipindi cha corona .

Anasema tatizo limeondoka na sasa maisha ya Watanzania yameendelea Kama kawaida kwa kufanya shughuli mbalimbali bila ya kuwa na hofu ya ugonjwa huo .

"Tunampongeza Rais kamtanguliza Mungu wakati wa kupambana na corona na sasa hali inaendelea vizuri na watu wanazidi kufanya shughuli zao za kimaendeleo bila kuhofu," anasema Ntemo.

Anazitaka shule zote ambazo zimenufaika na msaada huo, walimu wahakikishe wanasimamia vifaa hivyo ili kuwanusuru wanafunzi wasipate magonjwa ya milipuko na kutunza usafi wao ili wasome kwa furaha.

# Ni janga barakoa

**INATOKA UK.11**

Anasema, kusafisha mazingira kuna manufaa makubwa kwa afya ya wote katika kaya na katika jamii, hivyo ili kuepuka maradhi, ni muhimu kudumisha usafi kuanzia nyumbani.

"Niseme tu kwamba usafi wa mazingira unahusu pia kudumisha ratiba ya usafi, kwa kuhakikisha kuna kukusanya, kuondoa taka na majitaka au kuyatibu, kunawa kila wakati kabla ya kula, kunywa, kumaliza kutumia choo na hivyo usafi unatakiwa kuanzia nyumbani," Koshuma anasema.

Anafafanua kuwa mtu anayezingatia usafi nyumbani kwake, itakuwa rahisi kuepuka kutupa taka ovyo mitaani kama ambavyo baadhi ya watu wanafanya bila kujali kwamba ni hatari.

**WANAHITAJI KUELIMISHWA**

Kwa upande wa mkazi mtaa wa King'azi, jijini Dar es Salaam, Mariam Sanga anasema, ipo haja kwa jamii kuelimishwa jinsi ya kutunza mazingira na kuharibu au kutupa barakoa.

"Ninasema hivyo, kwa sababu wapo baadhi ya watu ambao hadi leo hukusanya taka mbalimbali kutoka nyumbani kwao na kuzitupa mitaroni badala ya kuchimba mashimo na kuzihifadhi," anasema Mariam.

Anakumbusha kuwa kuna wakati mwingine watu wanajisaidia haja ndogo katika chupa na kuzitupa popote au kujisaidia sehemu yoyote ambayo wanadhani ni uficho na kumbe wanachafua mazingira na kuhatarisha afya za wengine.

Hili tatizo ni kubwa hasa maeneo ya Uswahilini, watu wanajifanyia wanavyotaka, hivyo kuna haja ya kuwapa elimu watu wa aina hii ili waachane na mtindo huo wa kuhatarisha afya zao na za wengine," anasema.

Akiwa mjumbe wa nyumba 10, anafafanua kuwa anakutana na mambo mengi ambayo hufanywa na baadhi ya watu wasiozingatia usafi na kwamba amekuwa akipita nyumba kwa nyumba kuhimiza usafi.

AFYA

# 'Kuzaliwa bila jinsi hakunitishi'

**Na Elizabeth Zaya**

## • Hivi nilivyo nimejikubali • Naelekea kuwa mfamasia

BABY Musamba mkazi wa Kivule-Msongola Dar es Salaam, hivi karibuni alijitosa kwenye ubunge viti maalum-wenye ulemavu akijitangaza mbele ya wajumbe kuwa hana jinsi (sex). Si, mwanaume wala siyo mwanamke.

Kwenye mchuano huo aliambulia kura moja na kutupwa nje ya ulingo, pengine sasa anafikiria kujaribu tena miaka ijayo.

Maelezo haya yanaigusa Nipashe na kumsihi kuhojiana naye na katika maelezo yake, msichana huyo mwenye miaka 26 anaeleza kuwa kutokana na hali hiyo hajawahi kuwa na hisia za kimapenzi wala kutamani kuwa na uhusiano na hadhani kama itatokea kwenye maisha yake.

Licha ya kukosa jinsia wanaume wengi wanadhani kuwa ni mwanamke na mara nyingi wanamtaka kimapenzi lakini hafahamu cha kuwajibu na mara kwa mara anawapa ahadi za uongo.

Anasema bila kujali hali hiyo anamtumaini Mungu. Ameridhika vile alivyo, akisisitiza kuwa kumtumaini Mungu kuna faida kubwa kwani asipokuwa na moyo wa imani anaweza kukufuru.

### ANA TATIZO GANI?

Ili kufahamu kilichomsibu Nipashe inawasiliana mtaalamu wa afya daktari mbobezi wa masuala ya afya ya uzazi kwa kinamama (jina linahifadhiwa) akisema hali hiyo iliyompata Baby inajulikana kitabibu kama Disorder of Sex Development (DSD). Changamoto hiyo inatokana na viungo vya uzazi kushindwa kukomaa kama inavyohitajika.

Anasema pamoja na changamoto hiyo ipo aina nyingine ya hali hiyo inayoitwa Mayer-Rokitansky-Kuster-Hauser (MRKH) syndrome, ambayo mwanamke hukosa viungo vyote vya uzazi .

Hali hiyo hutokea mara chache kwa watoto wa kike, kwa wastani mtoto 1 kati ya 4,500 wanaozaliwa na husababishwa na mabadiliko katika vinasaba vinavyohusika katika ukuaji wa viungo vya mwanamke, anaeleza. Anasema mtu ambaye viungo vyake vya uzazi havijakua kikamilifu anaweza kufanyiwa upasuaji na vikarekebishwa na kwa yule ambaye hana viungo vya uzazi kama ilivyo kwa Baby, matibabu yake ni vigumu.

"Lakini kwa nchi za ng'ambo hufanya marekebisho na hata kumpandikiza mwanamke mji wa uzazi wa mtu mwingine na kutengeneza uke. Mhusika anaweza kuubeba ujauzito baada ya upasuaji na tiba ya kusisimua homoni,"anasema mtaalam huyo.

### HISTORIA YA BABY

Baada ya maelezo ya kitalaamu , Nipashe inarudi tena kwa Baby kufahamu namna alivyogundulika kuwa hana jinsi, akitoa maelezo anasema:

"Mama yangu alinieleza kwamba wakati anapewa taarifa ya kupata mtoto ambaye ni mimi, muuguzi wa kwanza alimweleza kuwa ana mtoto wa kiume wa pili akamwambia amejifungua msichana kwa hiyo, alibaki njia panda,"anasimulia Baby.



Baby Musamba. **PICHA: ELIZABETH ZAYA**

> **Wazazi wangu waliamua kunilea kama mtoto wa kike, kwa hiyo labda ndiyo maana nafanana hivyo, hata mimi napenda niwe hivyo.**

"Baadaye nilivyoletewa mtoto nikamwangalia na kushangaa nikawa sielewi nikarudi nyumbani. Baba naye alibaki anashangaa, kila mtu alikuwa haelewi ni mtoto wa aina gani na baadaye tuliamua kurudi hospitalini na kukabidhiwa daktari mbobezi wa watoto." Anaeleza akinukuu taarifa za mama yake.

Anasimulia kwamba baada ya kukabidhiwa kwa daktari, safari ya uchunguzi ilianza kwa kufanyiwa vipimo mbalimbali ili kufahamu ni mtoto wa kike au wa kiume, lakini vipimo havikuonyesha jinsi yoyote.

Anasema wazazi wake walisuibiri tena mpaka alipofikisha miaka miwili na kumpeleka tena hospitalini kwa ajili ya vipimo na uchunguzi zaidi.

"Niliendelea kupimwa mara kwa mara kila baada ya miaka kadhaa na hadi nilipofikisha miaka 20 nilikuwa napimwa tena, lakini hakukuonyesha dalili ya jinsi yoyote na ndipo madaktari waliposema hakuna uwezekano wowote kwa sababu tayari nimeshavuka umri wa udogo,"anasimulia Baby.

### ANALELEWA KIKE

Anasema baada ya vipimo kuonyesha kwamba si mtoto wa kike wala wa kiume, wazazi wake walichagua kumlea kama mwanamke, akivalishwa mavazi yote yanayowahusu wanawake.

"Wazazi wangu walinilea kwa upendo na umakini mkubwa na nilivaa kila aina ya nguo ya kike nionekane msichana japo sina matiti navaa sidiria,"anasimulia Baby na kwamba hata shuleni alijulikana kama binti japokuwa hayuko hivyo.

Baby anasema ingawa muonekano wake ni wa kike, lakini hana maumbile yoyote yanayomtambulisha kama wa kike isipokuwa anaamini anafanana hivyo kutokana na namna ambavyo wazazi wake waliamua kumlea.

"Wazazi wangu waliamua kunilea kama mtoto wa kike, kwa hiyo labda ndiyo maana nafanana hivyo, hata mimi napenda niwe hivyo," anasema Baby.

"Wazazi wangu walinishauri nisiwaambie watu jinsi nilivyo, walihofia kwamba ingeendelea kuniumiza na kunikatisha tamaa zaidi, kwa hiyo nilikuwa naishi kwa umakini ili wanafunzi wenzangu wasinigundue."

"Hakuna aliyenigundua hadi nilipomaliza darasa la saba na hata nilipokwenda sekondari mpaka kumaliza nako nilijificha sana hakuna aliyenifahamu ingawa nilisoma shule ya bweni, siri." Anasema na kuongeza:"Nilikuwa najitahidi kuwakwepa wenzangu hata inapofika wakati wa kuoga na ilipobidi kwamba tunaoga pamoja nilikuwa navaa nguo zangu za ndani."

### KUJIWEKA WAZI

Baby anasema mwaka 2014 Daktari wake alishauri kwamba ajiweke wazi badala ya kuendelea kuishi kwa kujificha.

"Daktari wangu alishauri inabidi tuvunje ukimya na ikiwezekana pendekezo lipelekwe hadi bungeni ili kama kuna watu wa aina yangu watambuliwe, kuthaminiwa na kusaidiwa lakini kwa kushauriana na kaka yangu tuliona ni bora katika kipindi hiki cha uchaguzi,"anasema Baby.

"Nilichukua kadi ya uanachama wa CCM siku nyingi lakini sikuwa hai kwa sababu nilikuwa nasoma na lengo lilikuwa ndiyo harakati za kujipanga kujiweka wazi baada ya ushauri wa daktari wangu,"anasema Baby.

Anasema ilipofika mwaka 2020 alijiamua kujitokeza kugombea ubunge kundi maalum la wenye ulemavu mkoa wa Dar es Salaam na kujiweka wazi.

Anasema baada ya kujitangaza kila mtu alishangaa na kila mmoja alitaka kuzungumza naye."Huwezi amini baada ya kujitangaza wengi walishtuka na kila mmoja alikuwa anataka kuzungumza na mimi muda uleule jambo ambalo lilikuwa haliwezekani,"anasema Baby.

### MALENGO YAKE

Baby anasema pamoja na changamoto hiyo anayoipitia hawezi kukata tamaa ya kutimiza ndoto zake na kwamba anasomea kozi ya ufamasia na kwamba analenga kufanya kazi katika sekta ya afya.

"Napenda mambo ya kutibu watu na masuala ya dawa, kwa sasa nasomea taaluma ya dawa ngazi ya diploma lakini nitaendelea kusoma zaidi kwa sababu lengo langu ni kuwatibu watu, napenda kuja kuwasaidia watu wenye changamoto kama zangu," anasema Baby.

### MAONI YA WANAFAMILIA

Frank Musamba ni kaka yake Baby anayesema kwamba wamezunguka kila mahali kutafuta tiba ya mdogo wake kwa zaidi ya miaka 20 tangu alipozaliwa, lakini ilifikia kipindi wakaamua kumwachia Mungu.

"Tumechukua hatua zote za kitabibu zinazojulikana mpaka imefika wakati tumesema tunamshukuru Mungu kwa hii hali, mpaka ka hapa alipo hakuna njia yoyote inayoweza kufanyika. Tunachotaka jamii pamoja na serikali ijue kamba watu wa namna hii wapo na wanahitaji kutambulika na kusaidiwa,"anasema Musamba.

MAZINGIRA

# Mabadiliko haya yanavyotishia hatima ya maskini hasa Afrika




Maeneo ya ufukweni ni miongoni mwa sehemu zitakazozama kutokana na ongezeko la joto duniani. Jitihada za kujenga kuta kukabili mawimbi ni hatua zinazochukuliwa kukabili mabadiliko. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mwandishi Wetu**

ATHARI za mabadiliko ya hali ya hewa zinakadiriwa kuwa mbaya mara tano katika miaka ijayo ikilinganishwa na hali ilivyo sasa. Katika nchi zinazoendelea joto kali linaweza kuwa tishio zaidi kwa maisha ya watu kuliko saratani na ugonjwa wa moyo.

Inakadiriwa kuwa mwisho wa karne ya 21 mamilioni ya watu wanaweza kufa kila mwaka duniani kwa sababu ya ongezeko la joto linalotokana na mabadiliko ya hali ya hewa.

Idadi hiyo ni kubwa na inaweza kufananishwa na kiwango cha vifo vinavyoweza kutokea duniani kutokana na magonjwa yote ya kuambukiza, ndivyo utafiti mpya unavyosema.

Utafiti huo unaonyesha kuwa viwango vya ' gesi chafu angani vitaendelea kuongezeka katika miongo kadhaa ijayo na litaongezeka zaidi na kusababisha vifo 73 kwa kila watu 100,000.

"Tunaona hatari inayowakabili watoto wetu wenyewe. Kijana wa miaka 10 aliyeko darasa la tano atafikia miaka 65 mwaka 2075, akikabiliwa na hatari ya kifo kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa kila mwaka baada ya kustaafu kwake."

> Kwenye maeneo ya pwani watu wanashuhudia mmomonyoko wa ukanda wa bahari unaotishia uharibifu wa miundombinu iliyopo katika maeneo hayo.

Wataalamu wanalinganisha kiwango cha sasa cha vifo vya magonjwa yote ya kuambukiza ikiwa ni malaria kifua kikuu (TB), VVU pamoja na maradhi yanayotokana na vimelea na virusi kuwa ni karibu vifo 74 kwa kila watu 100,000, duniani kote.

"Gharama kwa mataifa kutokana na ongezeko la joto duniani inaweza kuwa kubwa, kuna hatari ya vifo inayowakabili watoto. Kijana wa miaka 10 wa darasa la tano atafikia miaka 65 mwaka 2075, anakabiliwa na hatari ya kifo kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa kila mwaka atakapostaafu." Kwa mujibu wa ripoti za mabadiliko ya tabianchi mitandaoni.

Kupuuza kushughulikia mabadiliko ya hali ya hewa au tabianchi kunafananishwa na kuwaendesha watoto kwenye gari na kuacha milango wazi lakini pia bila kuwafunga mikanda na kushindwa kuwazuia kucheza kukielezwa kuwa huko ni kuweka maisha yao hatarini.

### MASKINI HATARINI

Tatizo la dunia kuwa na joto zaidi (kuwaka moto) linaelezwa kuwa litawaangukia na kuwaumiza zaidi watu masikini kwa maelezo kuwa takwimu zinaonyesha kuwa ukuaji endelevu wa uzalishaji wa gesi chafu, athari za ongezeko la joto zinakuwa na taathira mara tano katika mataifa yenye uchumi unaokua. Joto linaweza kuwa tishio zaidi kuliko saratani na magonjwa ya mengine yasiyoambukiza kwa mfano maradhi ya moyo.

Wataalamu wanaonya kuwa miji inayojengwa sasa haipo kwenye muundo wa kukabiliana na hali halisi ya mabadiliko ya tabianchi. Kinachoendelea ni kuzalisha utajiri wa kiuchumi kama kuweka viwanda vinavyozalisha moshi kwa wingi, magari yanayotumia petrol na dizeli, umeme unaozalishwa kwa dizeli, gesi na makaa ya mawe.

Miji imejengwa katika mazingira ya ulaji unaomaliza na kuondoa rasilimali za taifa, kuna upungufu wa kutumia na kuendeleza mazingira ya asili bila kujali kujiandaa kwa siku zijazo.

Kwa miongo mingi kumekuwa na uharibifu mkubwa wa mazingira hayo yanajidhihirisha kwenye ongezeko la joto ambalo sasa ni dhahiri kuwa ni kitisho.

Wakati viongozi wa dunia walipofanya mkutano Korea ya Kusini miaka miwili iliyopita walielezwa kuwa kuna uwezekano wa kuwapo na mabadiliko makubwa ya tabianchi wakati huu kama, inavyoelezwa na wanasayansi wa hali ya hewa.

Wakati wa kuelekea katika mkutano wa jopo la wanasayansi ambao utafanyika kwa miaka miwili huko Korea Kusini na kuangalia namna ambavyo dunia inakabiliana na ongezeko la joto ambalo huenda likafikia nyuzi joto 1.5 katika karne hii.

Hali hiyo inaelezwa kusababisha nchi nyingi zilizopo karibu na bahari kuwa na uwezekano mkubwa wa kupoteza miji yao iliyopo kwenye ukanda wa pwani.

Mwaka 2018 ulitajwa kuwa mwaka wa nne kuwa na joto ukilinganishwa na miaka mingine ya karne hii ya 20.

Kama udhibiti wa mabadiliko ya tabianchi hautapata muafaka inamaanisha kuwa uwekezaji mkubwa ambao umewekwa katika mataifa utapotea, kazi kubwa zikihusisha majengo, miundombinu na uwezekezaji vitaondoka hasa katika maeneo ya pwani na Tanzania pia itaathirika. Miji kama Dar es Salaam nayo ipo kwenye hatari ya kuzingirwa na maji na kupoteza rasilimali za gharama kubwa.

Rasilimali kubwa inayopatikana katika miji ya utalii kama Mombasa kwa mfano ambao umetajwa kuwa utapotea baada ya miaka 20 pengine kuanzia mwaka 2040 ni changamoto.

Mji huo kuzama baharini kunamaanisha athari kwa watu, bandari inayoongeza ukuaji wa uchumi wa Kenya na Afrika Mashariki.

Jambo ambalo ni muhimu kulizungumza kila wakati ni kulinda mazingira kwa vile mabadiliko ya tabianchi hayaonekani kwa siku moja bali huchukua miaka mingi lakini athari zake ni kubwa.

Kisiwani Pemba katika kisiwa cha Panza , maji yameanza kuzamisha kisiwa na yanasogea kwenda nchi kavu.

Aidha visiwa viwili kimoja mkoani Tanga wilayani Pangani na kingine cha Fungu la Nyani' mkoani Pwani nacho kimetoweka.

### ATHARI ZA MABADILIKO

Athari za mabadiliko ya tabianchi ambazo zinaonekana ni pamoja na kuongezeka kina cha bahari kutokana na kuyeyuka kwa barafu katika Bahari ya Arctic na Antactica.

Kwenye maeneo ya pwani watu wanashuhudia mmomonyoko wa ukanda wa bahari unaotishia uharibifu wa miundombinu iliyopo katika maeneo hayo.

Nyingine ni ongezeka la matukio ya vimbunga, upepo mkali, mathalani mwaka huu upepo ulivuma kwa miezi mitatu kluanzia Mei baada ya mvua za masika hadi sasa unasikika.

Aidha, kupungua kwa kasi kubwa kwa kiwango cha theluji katika vilele vya milima kama Kilimanjaro nayo ni athari, nyingine ni ukame wa mara kwa mara unaosababisha upungufu wa maji na kuenea kwa magonjwa kama vile malaria katika maeneo ambayo awali ugonjwa huo ulikuwa haupo. **MITANDAO**



# Wagombea waaswa kwenda kwa waganga wa kienyeji

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAGOMBEA wa nafasi mbalimbali kwenye uchaguzi mkuu mwaka huu, wametakiwa kuacha kupoteza muda wao kuhangaika kwa waganga wa kienyeji ili wachaguliwe.

Mwenyekiti wa Shirikisho la Vyama vya Waganga wa tiba asili Mkoa wa Dodoma, Issa Mdoe, alitoa rai hiyo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kwenye Wiki ya Maadhimisho ya Tiba Asili ya Mwafrika kitaifa yaliyoandaliwa na Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto yaliyofanyika jijini hapa.

Alisema Tanzania inawahitaji viongozi wenye sifa na uwezo wa kuongoza na walio na maadili ya kimungu na si kujihusisha na imani za ushirikina na watoa rushwa.

Mdoe alisema Watanzania watamchagua mgombea kulingana na sifa za elimu na sera za vyama vyao na si kwa kupewa hirizi kwa waganga wa kienyeji.

Aidha, mwenyekiti huyo aliwataka wagombea hao kumtegemea Mungu badala ya waganga wa kienyeji kwa kuwa wanaweza kujikuta wakipoteza fedha na nafasi wanazozihitaji.

"Mimi nikiwa kama kiongozi wa shirikisho la vyama vya waganga wa tiba asili, nasema wakija hao viongozi na fedha na mali zao hatutaacha kupokea, lakini wasitegemee kupata nafasi wanazoziomba bali waombe kwa Mwenyezi Mungu na sivyo vinginevyo," alisema.

Aliwahimiza wagombea kutumia elimu waliyonayo kuelezea sera za chama husika badala ya kutishiana na kutoa lugha ambazo zimekuwa zikiharibu ustaarabu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Cornwell Tanzania, Dk. Elizabeth Lema, aliwaomba Watanzania kutunza miti ya asili kwa kuwa ndio mahala ambapo dawa zinapatikana.

Alisema baadhi ya maeneo mbalimbali ndani ya nchi miti shamba imeanza kuadimika kutokana na kukatwa ovyo.

"Zamani kulikuwa na miti ambayo ilikuwa na faida nyingi kwa matumizi ya wanadamu katika kutengeneza bidhaa mbalimbali zikiwamo dawa za tiba asili pamoja na pafyumu, lakini leo hii huwezi kupata hiyo miti," alisema.




Mratibu wa selimundu katika Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Asteria Mpoto, akizungumza wakati wa uzinduzi wa mwezi wa kuelimisha jamii kuhusu ugonjwa wa selimundu, uliofanyika jijini Dodoma juzi. Kulia ni Daktari Bingwa wa magonjwa ya damu, Dk. Stella Mlangahe. **PICHA IBRAHIM JOSEPH**

# DC afichua siri matokeo mazuri shule Mpwapwa

**Na Augusta Njoji,** MPWAPWA

MKUU wa Wilaya ya Mpwapwa, Jabir Shekimweri, amefichua siri ya shule nne za kidato cha sita kwenye wilaya hiyo kupata matokeo mazuri.

Sababu hizo amezitaja kuwa ni pamoja na ushirikiano, kujituma kati ya wanafunzi, walimu na wazazi.

Kutokana na hilo, amewataka kutobweteka bali waendelee kushirikiana zaidi ili kupata matokeo mazuri yatakayoipaisha wilaya hiyo kielimu.

Akizungumza jana na Nipashe, Shekimweri alisema wilaya hiyo ina shule nne za kidato cha tano na sita, ambapo katika matokeo ya mitihani ya kidato cha sita uliofanyika Juni 2020, wanafunzi 92 wamepata daraja la kwanza.

"Katika shule hizo nne ambazo ni Kibakwe, Berege, Mazae na Mpwapwa, wanafunzi 175 wamepata daraja la pili, wanafunzi 102 wamepata daraja la tatu, wanafunzi wanne wamepata daraja la nne na aliyepata sifuri ni mwanafunzi mmoja pekee, haya ni mafaniko makubwa sana," alisema Shekimweri.

Aliwapongeza wananchi wa Mpwapwa kwa mwamko wao katika elimu, mkurugenzi, Idara ya elimu sekondari, walimu na wanafunzi kwa kujituma kwao kila mmoja kwa nafasi yake, hivyo kupata ufaulu huo.

"Kwa namna ya pekee kabisa niipongeze Shule ya Sekondari ya Berege, hii shule ni ya Kata ambayo Rais John Magufuli aliipandisha hadhi (sawa na Mazae na Kibakwe kwa lengo la kupokea wanafunzi wa kidato cha tano na sita.

"Leo ninafurahi kwamba mwanafunzi wake mmoja, Halord Sanja, ameingia kwenye kundi la wanafunzi kumi mahiri wa somo la Kiswahili, hatua hii ni ya kupongezwa sana," alisema Shekimweri.

Alisema mafanikio yote yanapatikana kutokana na uwekezaji mzuri uliofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano ya kuboresha sekta ya elimu upande wa miundombinu ambapo shule zote hizo.

Alibainisha serikali imetoa zaidi ya Sh. billioni mbili ambazo zimetumika kujenga hosteli, bwalo la chakula na maktaba ikiwamo ukarabati wa shule kongwe ya Mpwapwa Sekondari.

Aidha, alisema uwezeshaji wa nyenzo za kufundishia na kujifunzia, ushirikiano wa wadau pamoja na hamasa au motisha kwa walimu vimechangia sana kuongeza ufaulu.

# 'Pimeni selimundu kabla ya mahusiano'

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WATANZANIA wameshauriwa kupima vinasaba (DNA) vya ugonjwa wa selimundu kabla ya kuingia kwenye mahusiano ili kuzuia kupata watoto wenye ugonjwa huo.

Hatua hiyo, imetokana na kila mwaka watoto 11,000 nchini wanazaliwa na ugonjwa huo na hivyo Tanzania kukabiliwa na idadi kubwa ya wagonjwa ikilinganishwa na nchi zingine duniani.

Daktari bingwa wa magonjwa ya damu kutoka Hospitali ya Benjamin Mkapa, Dk. Stella Malangahe, alitoa ushauri huoo kwenye uzinduzi wa mwezi wa kuelimisha jamii juu ya ugonjwa huo.

"Ugonjwa wa sickle cell unazuilika, nawashauri wenza kabla ya kuingia kwenye mahusiano wanapaswa kufanya vipimo vya kubaini vinasaba vya ugonjwa huo ili kuzuia kupata watoto wenye selimundu," alisema.

Alisema ugonjwa huo husababisha athari mbalimbali ikiwamo ini, figo, mapafu, kupooza na vifo vya mapema.

Alisema kuwa mtu mwenye ugonjwa wa selimundu huongezewa damu mara kwa mara kwa sababu chembe chembe nyekundu za damu zao haziwezi kukaa muda mrefu.

"Kukiwa na mgonjwa wa selimundu basi lazima mama au baba yake ana ugonjwa huo, dalili za ugonjwa huu ni maumivu ya mara kwa mara, kuvimba miguu, mikono na hasa mtoto anapokuwa ametimiza miezi sita, kulia sana na kupata manjano mikononi na miguuni, kupungukiwa damu mara kwa mara," alisema.

Hata hivyo, alisema licha ya ugonjwa huo kuwa tishio, kwa sasa unatibika ambapo mgonjwa anawekewa uboho wa ndugu wa karibu ambaye hana historia ya ugonjwa huo.

Akizindua mwezi wa maadhimisho ya ugonjwa huo ambao hufanyika Septemba 1-9, kila mwaka, Kaimu Mkurugenzi wa Tiba, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Sarah Maongezi, alisema watoto 1,000 huzaliwa na ugonjwa huo kila siku duniani, huku 11,000 huzaliwa kila mwaka Tanzania.

Alieleza kuwa Tanzania ni nchi ya tano duniani kuwa na idadi ya wagonjwa wengi na inashika nafasi ya nne barani Afrika.

"Nchi zenye wagonjwa wengi duniani ni Nigeria, India, DRC, Angola na Tanzania ambapo kwa Afrika Tanzania inashika nafasi ya nne, hali inayopaswa kutiliwa mkazo zaidi kuhakikisha ugonjwa huu unadhibitiwa," alisema.

Alisema kila watoto 100 wanaozaliwa nchini, wanane kati yao wana ugonjwa huo, huku akisema juhudi nyingi zinazofanywa na Wizara ya Afya ni kuelimisha jamii juu ya ugonjwa huo. "Jamii bado haina uelewa wa kutosha, hali inayosababisha unyanyapaa kwa waathirika wa ugonjwa huo," alisema.





# Wataalamu tiba asili watakiwa kujisajili

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATAALAMU wa tiba za asili katika mkoa wa Mbeya, wametakiwa kusajili huduma zao ili watambulike kwa mujibu wa sheria na kuepuka kuchukuliwa hatua za kisheria pale yanapotokea matatizo kwenye huduma hizo.

Hayo yalisemwa juzi na Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Salum Manyatta, alipokuwa anazungumza na wataalamu hao wakati wa maadhimisho ya Siku ya Tiba za Asili huku akibainisha kuwa takwimu zinaonyesha zaidi ya watoa huduma 3,000 hawajasajiliwa.

Alisema serikali imeweka utaratibu wa kusajili shughuli hizo ili kuzifanya zitambulike na kurasimishwa ili zitumike kama ilivyo kwenye mataifa mengine ambayo ziko hospitali zinazotoa huduma kwa kutumia mitishamba.

Huduma hizo za tiba za asili, alisema ni kama maduka ya dawa za binadamu ambayo hayawezi kufanya kazi bila kusajiliwa, hivyo akawasisitiza wataalamu wa huduma hizo kuzingatia sheria za nchi ili kuepuka kushughulikiwa.

"Mnatakiwa mhamasishane wenyewe kujisajili. Ukiona mwenzio anatoa huduma bila kusajiliwa ujue anakuharibia na wewe kazi yako. Sasa utaratibu uko wazi na ni rahisi kabisa, naomba sana mjitahidi ili kazi zenu zitambulike na zikuwe," alisema Dk. Manyata.

Alisema utaratibu wa kusajili huduma hizo unaanzia katika ofisi za watendaji wa mitaa na kata mpaka katika ngazi ya wilaya ambako ndiko vibali vinatolewa na kwamba kwa sasa huduma hizo zinafanyika kielektroniki.

Dk. Manyatta alisema mtoa huduma akishasajiliwa anakuwa anatembelewa na maofisa wa halmashauri ambao huwa wanakagua ubora wa huduma na mazingira ya kutolea

# Askofu ataka Watanzania kumtanguliza Mungu

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

WATANZANIA wameshauriwa kuiga mfano wa Rais John Magufuli, kumtanguliza Mungu kila wanapofanya shughuli zao ili awaepushe na matatizo yanayoweza kuwakabili kwenye maisha yao.

Askofu Mkuu wa Kanisa la Moravian Tanzania, Joseph Mwambungu, alitoa ushauri huo mwishoni mwa wiki katika Ushirika wa Kyela mkoani Mbeya alipokuwa anatoa shukurani kwa uongozi wa kanisa hilo kumsimika kushika wadhifa huo wa juu ndani ya kanisa.

Alisema mara nyingi Rais Magufuli amekuwa akionekana kwenye makanisa na misikiti mbalimbali akihudhuria ibada liche ya kuwa yeye ni kiongozi mkuu wa nchi na kwamba, lakini baadhi ya watu wasiokuwa na wadhifa wowote wanashindwa kuhudhuria ibada wakidai kuwa wanakosa muda.

Mwambungu alisema dunia sasa inakabiliwa na matatizo mbalimbali ambayo yanahitaji kumshirikisha Mungu ili kuyaepuka na kwamba Rais Magufuli ameonyesha mfano wa kufanya hivyo, kwa hiyo inafaa kila Mtanzania kuiga mfano huo.

"Leo hii ndani ya nchi yetu, corona imekuwa kama historia kwa sababu kiongozi wetu alituongoza kumwomba Mungu. Baadhi ya mataifa sasa hivi bado ugonjwa huo umekuwa tatizo kubwa sana, lakini sisi tunaendelea na shughuli zetu na wengine wameacha hata kufuata zile taratibu," alisema Askofu Mwambungu.

Alisema yawezekana baadhi ya watu wanashindwa kufanikiwa kwenye shughuli zao kwa sababu hawana hofu ya Mungu ndani yao na wamshirikishe kwenye kila jambo. Mwambungu aliushukuru uongozi wa kanisa hilo kwa kumteua yeye kuwa kiongozi wa juu wa kanisa na kwamba atahakikisha analitumikia kanisa hilo kwa weledi na kushirikiana na serikali kwenye utekelezaji wa baadhi ya shughuli.

Akitoa salamu za serikali katika ibada hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Cloudia Kitta, alisema serikali itaendelea kushirikiana na viongozi wa dini katika shughuli mbalimbali za maendeleo. Aliwaomba viongozi wa dini nchini kuendelea kuliombea taifa hasa katika kipindi hiki cha kuelekea Uchaguzi Mkuu ili amani iliyopo iendelee kudumu na nchi iendelee kupata maendeleo.

Kitta alisema mara nyingi Rais Magufuli amekuwa akiwaalika viongozi wa dini kwenye shughuli mbalimbali za kiserikali kutokana na kutambua umuhimu wao kwenye maendeleo, hivyo akawaomba waendelee kuiunga mkono serikali.

"Nakupongeza sana Askofu Mwambungu kwa nafasi hiyo uliyoaminiwa. Ni matumaini yangu kuwa utaliongoza kanisa katika misingi inayotakiwa, lakini mchango wako kwa serikali utahitajika sana hasa kwenye uhamasishaji wa shughuli za maendeleo," alisema Kitta.



Mgombea ubunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Oran Njeza (kushoto), akipokea kitabu cha ilani ya uchanguzi ya chama hicho, kutoka kwa Katibu Mwenezi wa CCM Mkoa wa Mbeya, Bashiru Madodi, wakati za uzinduzi wa kampeni za ubunge na madiwani wa chama hicho, katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Aagiza klabu ya Ukimwi kusaidiwa

**Na Nebart Msokwa,** MBOZI

SERIKALI imeliagiza Shirika la Watu Wanaoishi na Virusi vya Ukimwi nchini (NACOPHA) Kanda ya Mbeya, kuilea Klabu ya Ukimwi na Mazingira (UTU) ya wanafunzi wa Shule ya Msingi Itete iliyoko Kata ya Mlowo, Mbozi mkoani Songwe ili iwe endelevu.

Katibu Mkuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Uwekezaji, Doroth Mwaluko, alitoa agizo hilo alipotembelea klabu hiyo ya wanafunzi na vikundi mbalimbali vya watu wanaoishi na Virusi vya Ukimwi (VVU) mkoani hapa.

Alisema klabu hiyo ni miongoni mwa makundi muhimu kwenye vita dhidi ya Ukimwi katika mkoa kutokana na hamasa ambayo watoto hao wanaitoa kwa jamii kuhusu ugonjwa huo, hivyo ni lazima iendelezwe. Mwaluko alilitaka shirika hilo kushirikiana na uongozi wa shule hiyo kwenye malezi ya kikundi hicho ikiwa ni pamoja na kuwapatia elimu ya kutosha kuhusu Ukimwi ili wanapohamasisha wawe wana uelewa wa kutosha kuhusu ugonjwa huo.

"Hawa watoto wana maono mazuri na ni kundi muhimu sana kwenye hii vita dhidi ya Ukimwi. Lakini hapa kinachoonekana wamekosa usaidizi wa kuwaimarisha, sasa natoa agizo kwa NACOPHA hakikisheni mnailea hii klabu, huu ni msingi mzuri sana." aliagiza Mwaluko.

Aliwataka watoto hao kuhakikisha wanakiishi kile wanachohamasisha jamii ikiwamo kuepuka kuanza kushiriki mapenzi wakiwa bado na umri mdogo ili kuepuka kupata maambukizi ya VVU kwa maelezo kuwa elimu wanayoitoa itakuwa haina maana.

Mwaluko alisema ili mapambano ya Ukimwi yawe na mafanikio, wazazi wanatakiwa wawe na ujasiri wa kuzungumza na watoto wao kuhusu ugonjwa huo ambao alisema unapunguza nguvu kazi ya taifa. Awali, Mwenyekiti wa Klabu hiyo, Lucy Nyale, alisema klabu ilianzishwa mwaka 2014 na ikasajiliwa rasmi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi mwaka 2017 baada ya kushauriwa na kamati na kwamba hapo ndipo shughuli zao zilipoanza kutambulika.

Alisema klabu ina wanachama 48 ambao 40 ni wasichana na wanane pekee ndio wa kiume, huku akidai kuwa idadi ya wavulana ni ndogo kutokana na kuwa wagumu kujiunga kwa sababu wanaogopa kuwa wakijiunga watapimwa afya zao. Mbali na kutoa elimu ya Ukimwi kwa jamii, pia alisema klabu inajishughulisha na biashara ambapo alidai inamiliki duka la vifaa vya shule ambavyo wateja wake wakubwa ni wanafunzi na walimu.

Vilevile alisema klabu hiyo inashughulika na utoaji wa elimu ya kuhamasisha utunzaji wa mazingira pamoja na kuhamasisha utalii ndani ya mkoa wa Songwe.

"Tuna mradi wetu wa kuwasaidia wanafunzi wenzetu ambao wanaishi katika mazingira magumu kwa kuwapatia uji wa lishe ili waimarishe afya zao, lakini tatizo linalotukabili ni ukosefu wa mtaji wa kutosha kwa ajili ya kuendesha shughuli zetu," alisema Lucy.

# Mwinyi ataka wasomi kuibua sera za maendeleo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MGOMBEA wa urais wa Zanzibar kupitia tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Hussein Mwinyi, amewataka vijana wasomi wa chama hicho kuibua sera ambazo zitasaidia kuleta maendeleo na kupiga hatua kubwa za kiuchumi kwa ajili ya kuzalisha ajira.

Dk. Mwinyi alisema hayo wakati akihutubia mdahalo wa vijana wasomi wa vyuo vikuu huko Tunguu katika ukumbi wa Dk. Ali Mohamed Shein, Mkoa wa Kusini Unguja.

Alisema tatizo la ajira ni kubwa, lakini njia pekee ya kulipatia ufumbuzi ni kuwekeza katika viwanda na uvuvi wa bahari kuu.

Alisema hadi sasa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Zanzibar, bado haijatumia vizuri eneo la bahari kuu ambalo ni kubwa lenye utajiri mkubwa wa rasilimali za viumbe vya baharini.

Alisema njia pekee ya kutumia rasilimali hizo ni kuweka sera nzuri pamoja na sheria ambazo zitawawezesha wananchi kuvuna na kufaidika na fursa hizo kikamilifu.

"Nyinyi vijana ndiyo tegemeo kubwa la kuibua sera ambazo zitasaidia kuwapo kwa sheria nzuri za kufaidika na rasilimali zilizopo nchini...tumezungukwa na bahari pande zote, lakini hatujaweza kulifikia eneo la bahari kuu na kuvuna rasilimali zilizopo," alisema.

Naye Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo Kikuu cha Mwalimu Nyerere, Dk. Razak Lukina, aliitaka Serikali ya Zanzibar kuwekeza katika uvuvi wa bahari kuu wenye utajiri mkubwa wa rasilimali ambazo hazijatumika kikamilifu kwa ajili ya kulinufaisha taifa na watu wake.

Alisema uchumi wa bahari unakuwa kwa asilimia nne kwa mwaka huu zaidi ya Shilingi trilioni tatu zikipatikana kwa uvuvi wa samaki wa aina mbalimbali ikiwamo jodari, kwa upande wa Zanzibar mapato yanayotokana na uvuvi wa bahari ni asilimia mbili.

"Bado Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haijatumia vizuri utajiri wa rasilimali zinazopatikana baharini ikiwamo uvuvi wa bahari kuu wenye tija utakaosaidia kuzalisha ajira," alisema.

Mwenyekiti wa Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA), Dk. Zakia Abubakar, aliwataka vijana kujitambua na kufahamu umuhimu wa kupiga kura kuelekea uchaguzi mkuu ambayo ni haki ya kidemokrasia.

Alisema vijana wakishiriki kikamilifu katika mchakato wa uchaguzi mkuu ikiwamo harakati za kampeni kwa kiasi kikubwa wanaweza kufahamu malengo ya wagombea na nia zao hivyo kufanya maamuzi sahihi.

"Vijana tunaelekea katika uchaguzi mkuu kwa Oktoba 28... tunatakiwa kufanya maamuzi sahihi ya kuwachagua viongozi wenye sifa na uwezo wa kuongoza nchi," alisema.

Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Vijana (UVCCM), Mussa Haji Mussa, alisema matarajio makubwa ya vijana yapo kwa mgombea wa CCM, Dk. Hussein Mwinyi, ambaye ameonyesha uwezo mkubwa wa kuzipatia ufumbuzi changamoto zinazolikabili kundi hilo. "Tumemsikia mgombea wa urais wa Zanzibar kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi Dk. Hussein Mwinyi...huyu ndiye chaguo sahihi la kuzipatia ufumbuzi changamoto zinazowakabili vijana ikiwamo ajira.



Baadhi ya wananchi wakiwa wamepanga foleni katika kituo cha kununua umeme eneo la Mazizini mjini Zanzibar juzi, baada ya huduma hiyo, kukosekana kwa njia ya mtandao wa simu. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Waganga tiba asilia watakiwa kufuata maadili

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAGANGA wa tiba asili na tiba mbadala wametakiwa kufuata miiko na maadili ya kazi zao, ili kuepukana na changamoto wakati wanapofanya kazi zao.

Hayo yalielezwa na Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ayoub Mohammed Mahmoud, katika kisiwa cha Uzii kwenye maadhimisho ya sherehe za waganga wa tiba asili na tiba mbadala, barani Afrika.

Alisema kumekuwapo na wimbi kubwa la waganga wanaokiuka misingi ya kazi zao hali inayosababisha jamii kukosa imani na tiba hiyo. Alisema waganga wa tiba asili na tiba mbadala wana mchango mkubwa wa kuisaidia serikali kuhakikisha inapunguza gharama za kuagiza dawa kutoka nchi za nje endapo watafanya utafiti wa miti iliyopo nchini kwa lengo la kutoa tiba kwa wananchi.

Alisema historia inaonyesha kuwa tiba hizo zilikuwapo tangu zamani na zimesaidia kutibu magonjwa mbalimbali kwa mafanikio makubwa.

Aliitaka Jumuiya ya Waganga Zanzibar (JUTIJAZA), kuangalia uwezekano wa kuwapa hadhi waganga ambao wanafanya kazi kwa kufuata sheria na taratibu ili kuwatambua waganga hao na ambao wanafanyakazi kwa kubahatisha. Naye Mwenyekiti wa Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala Zanzibar, Dk. Mayasa Salum, alisema katika kuboresha huduma za tiba asili na mbadala, baraza limeweka mikakati mbalimbali kwa lengo la kuhakikisha wataalamu wa tiba hizo wanakuwa na dira, mwelekeo na kuziboresha huduma zao kama ilivyo katika nchi zilizoendelea ikiwamo India, nchi za kiarabu na mataifa mengine duniani.

Hata hivyo, alisema serikali kupitia Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala inaendelea na juhudi za kuwaunganisha waganga wote wanaofanya kazi zao nchini licha ya uhaba wa rasilimali fedha na vifaa hali inayowafanya washindwe kuwafikia waganga hasa wa vijijini na kusababisha idadi kubwa ya waganga ambao hawajasajiliwa.

Akisoma risala ya waganga hao, Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Waganga, Haji Juma Msanif, alisema mbali ya mafinikio makubwa yaliyopatikana kwa miongo miwili ya tiba asili barani Afrika, zipo changamoto mbalimbali zinazoikabili jumuiya hiyo ikiwamo kukosa uwezeshaji wa kuziingiza dawa kwenye mfumo wa kisasa na kukosa chuo cha utafiti wa dawa za asili.

# Serikali kutoa mikopo mil. 800/- kwa wajasiriamali

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Kazi, Wazee, Wanawake na Watoto, kupitia Mfuko wa Uwezeshaji imejipangia kutoa mikopo 700 kwa vikundi vya kiuchumi na wajasiriamali yenye thamani ya Sh. milioni 850 kwa sekta zote za kiuchumi katika mwaka wa fedha 2020/2021.

Waziri wa Wizara hiyo, Mouldine Syrus Castico, aliyasema hayo juzi wakati wa uzinduzi wa Jukwaa la Wanawake milioni 50 wa kiafrika, liliofanyika mjini hapa.

Alisema kuwa takwimu za kiuchumi duniani zinaonyesha kuwa sekta ya ujasiriamali imeendelea kukua na hivyo kutoa mchango mkubwa wa maendeleo ikiwamo kuzalisha ajira.

Alisema kuwa mwaka wa fedha 2019/2020 mfuko huo ulitoa mikopo 811, Unguja na Pemba yenye thamani ya Sh. milioni 789.35 kwa wajasiriamali mbalimbali.

Kati ya hiyo, mikopo ya vikundi ni 223, vikiwamo 42 vya makundi maalumu ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu na vilivyobakia 181 ni vikundi mchanganyiko.

Castico alisema jumla ya wajasiriamali 5,092 walinufaika na mikopo hiyo, kati ya hao wanawake ni asilimia 53.

Alisema uzinduzi wa jukwaa hilo umefanywa kwa lengo la kuwahamasisha wanawake kufanya biashara kwa njia ya kimtandao, kupanua zaidi na kuelekea kwenye mtandao wa Afrika Mashariki na kufikia mtandao wa kikanda na kimataifa.

Aliishukuru Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kuratibu utekelezaji wa mradi huo, ambao ni muhimu kwa maendeleo ya wanawake na wajasiriamali nchini.

Alisema katika takwimu za dunia za mwaka 2014 zinaonyesha asilimia 80 ya Wazanzibari wapo katika sekta hiyo, 47 ya wajasiriamali wanawake wanaojishughulisha na biashara.

Naye Katibu wa masuala ya kijamii kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki, Christopher Bazisamo, aliwataka wanawake wa kizanzibari kuchamgamkia fursa hiyo ambayo ni maalumu kwao katika kujiendeleza kiuchumi.

Alisema pamoja na kuwa fursa hiyo ni muhimu wanatambua kuwa kuna changamoto ya upatikanaji wa vifaa vya kidijitali ambavyo jumuiya inalifanyia kazi.

Pia alisema kuwa pamoja na kuwa mradi huo unawahusu wanawake pekee, lakini wanaume wanaweza kuingia ili kuona biashara zinazofanywa zinanunuliwa.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA/MASHAMBA

**KIWANJA KINAUZWA, K**IWANJA CHA COMMERCIAL 1300SQM KINAUZWA KIPO REGENT ESTATE HAKUNA DALALI TUPIGIE: 0693 689996/ 0757 129546

**KIWANJA KINAUZWA,** Kipo ukonga kitunda Mwanagati Ukubwa 3175sqm kandoni mwa barabara kubwa kimepimwa kinafaa kwa shughuli yeyote utakayo ujirani mzuri, Lorry kubwa kinaingia Bei ni 75 mil. Mawasiliano: 0719 619 444/ 0782 574 669


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676


## KUPOTEA KWA VYETI



**Philipo Chombo** anatangaza kupotea kwa vyeti vifuatavyo cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0351/0149** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2003 katika shule ya Sekondari Bagamoyo, cheti cha ualimu chenye index namba **E505/173** kilichotolewa mwaka 2005 na chuo cha Ualimu Korogwe. Yeyote atakaeiviona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **KOR/B.I/27/VO.IV/32/2011**

115883102

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;251/2020**

**Ombi la NEEMA MOUSA BALATI,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu MOUSA TONTO BALATI.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 05/10/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 02/09/2020.

MAHAKAMA YA MWANZO MOROGORO MJINI

Tarehe 2/9/2020

Sahihi ya Hakimu

HAKIMU MAHAKAMA YA MWANZO MJINI MOROGORO

215883502

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI KWA MDAIWA**

**MAHAKAMA YA MWAZO NYANKUMBU WILAYA YA GEITA**

**SHAURI LA MADAI NA. 46/2020**

**MDAI: SALA SAMWEL**

**DHIDI YA**

**MDAIWA: PANTALEO WAZIRI WA TAMBUKALELI**

**AMRI:** Unaamriwa na Mahakama uhudhurie hapa Mahakamani mnamo tarehe 4/9/2020 saa 2:30 asubuhi bila kukosa. Usipohudhuria shauri hili laweza kusikilizwa upande mmoja bila ya wewe kuwepo, na kutolewa uamuzi. Hati hii imetolewa kwa amri yangu na muhuri wa Mahakama leo JUMATANO tarehe 26/8/2020.

HAKIMU

115883702

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**

**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI YA 2)**

**Katika mahakama ya mwanzo DODOMA MJINI**

**Usimamizi wa mirathi 109/2020**

**Ombi la SAMANTHA SEBASTIAN kuteuliwa Msimamizi wa mirathi Marehemu SEBASTIAN STEVEN KINABO**

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA TANZANIA BARA.**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 04/09/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo. Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 01/9/2020

COURT SEAL URBAN COURT DODOMA DISTRICT

Tarehe

Sahihi ya Hakimu

PRINCIPAL PRIMARY COURT MAGISTRATE URBAN DODOMA

115883902

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**CENTRE FOR SUSTAINABLE DEVELOPMENT INITIATIVES** INATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA TOYOTA LAND CRUISER YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 697 AEW.** KWA YOYOTE ATAKAYE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **DAR/OST/RB/638093/2020.**

115883802

---

ROCK TAKERS LTD

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

**SHAURI LA JINAI NO.201/2020**

**NICHOLAUS ELISHA KISSI ....................MLALAMIKAJI**
**DHIDI YA**
**LEONARD NCHUBA ................................MSHTAKIWA**

**SHAURI LA MIRATHI NO.55/1999**

**SAIDATY MWEDADI .............................. MWOMBAJI**
**HASSAN RASHID SALUM .......................MWOMBAJI**

**DC MATRIMONIAL CASE NO. 04/2019**

**GABRIEL MASUMBUKO JOSEPH..................... PLAINTIFF**
**VS**
**PERPETUA CHAUSIKU GEORGE.................. DEFENDANT**

**KWA IDHINI NA MAMLAKA TULIYOPEWA NA MAHAKAMA YA MWANZO YA NYAMAGANA, MAHAKAMA YA MWANZO YA MKUYUNI NA MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI MKOA TUTAUZA KWA MNADA WA HADHARA MALI ZA MSHTAKIWA, MAREHEMU NA WANANDOA AMBAZO NI NYUMBA MNADA UTAFANYIKA MAHALA MALI ILIYOKO.**

| SN | MALI INAYOUZWA | MAHALI | MUDA |
|---|---|---|---|
| 1 | NYUMBA KWENYE KIWANJA NA. 901 KITALU "A" | BUHONGWA | 17/09/2020 SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 2 | NYUMBA NA. 017/094 NA GARI (NOAH) T. 317 BJX | TAMBUKARELI – BUTIMBA | 17/09/2020 SAA 8 MCHANA NA KUENDELEA |
| 3 | NYUMBA YA WANANDOA | NYAKATO, MAHINA - NYAMAYUKI | 18/09/2020 SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA:**

1. MTEJA ATALIPA ASILIMIA ISHIRINI NA TANO YA BEI ITAKAYOFIKIWA KWENYE MNADA NA ITAKAYOSALIA ATAILIPA NDANI YA SIKU KUMI NA NNE,KUSHINDWA KUFANYA HIVYO MTEJA ATAKUA AMEPOTEZA HAKI YAKE YA MSINGI NA MNADA UTARUDIWA TENA.
2. GHARAMA ZOTE ZITAKAZOJITOKEZA BAADA YA KUNUNUA MALI KWENYE MNDA NI JUU YA MNUNUZI.

**MAWASILIANO: 0713 342969/0627 672221**


**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe MWANGA WA JAMII

**Uza,**

**Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza**

**Nasi Kwa Bei Poa**

**Tupigie 0782253676**


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Sumu ya nyuki kutibu saratani ya matiti

**CANBERRA,** Australia

WANASAYANSI nchini Australia wanasema kwamba sumu ya nyuki wanayotengenezea asali ina uwezo wa kuharibu seli hatari za saratani ya matiti katika maabara.

Sumu hiyo ina kemikali aina ya melitin, ilitumika dhidi ya aina mbili ya saratani ambazo ni ngumu kutibu.

Ugunduzi huo umetajwa kuwa wa kufurahisha, lakini wanasayansi wametoa tahadhari kwamba vipimo zaidi vinahitajika. Saratani ya matiti imeelezewa kuwa ndiyo ambayo inawaathiri wanawake wengi duniani.

Huku kukiwa na maelfu ya kemikali zinazoweza kukabiliana na seli za saratani katika maabara, wanasayansi walisema kwamba kuna chache zinazoweza kuzalishwa kama tiba ya wanadamu.

**Inatoa mfano mzuri wa ni wapi kemikali asilia zinaweza kutumika kutibu ugonjwa unaoathiri wanadamu.**

Awali, sumu ya nyuki ilibainika kuwa na tiba dhidi ya aina nyingine ya saratani kama ile ya Melanoma.

Utafiti huo wa taasisi ya Harry Perkins kuhusu tiba Magharibi mwa Australia ulichapishwa katika jarida la asilia.

Mtafiti Ciara Duffy (25) ambaye aliongoza utafiti huo, alisema walifanyia vipimo sumu za nyuki 300, kutoka kwa nyuki wa kutengeneza asali na zilionekana kuwa na uwezo mkubwa.

Sumu hiyo kali iligunduliwa kuwa na uwezo wa kuua seli za saratani ndani ya saa moja, bila kudhuru seli nyingine.

Lakini sumu hiyo iliongezeka viwango vingine vya tiba.

Utafiti huo pia ulibaini kwamba kemikali ya Meltin ilikuwa na uwezo mkubwa katika kuua au kuharibu ukuaji wa seli za saratani.

Huku Meltin ikiwa ndani ya sumu ya nyuki wa asali pia inaweza kuzalishwa katika maabara.

Jumatano, wanasayansi kutoka Australia Magharibi walielezea utafiti huo kama wa kufurahisha.

Prof. Peter Klinken alisema utafiti huo unaonyesha kwamba Meltin inaingilia ukuaji wa seli za saratani ndani ya matiti ili kuzuia kuzaana kwa seli hizo.

“Inatoa mfano mzuri wa ni wapi kemikali asilia zinaweza kutumika kutibu ugonjwa unaoathiri wanadamu,” alisema.

Lakini watafiti hao wanaonya kwamba kazi zaidi inahitajika kuona iwapo sumu inaweza kutumika kwa kiwango gani kama tiba ya saratani.

Prof. Alex Swarbrick kutoka taasisi ya tiba ya Sidney alisema wanakubali kwamba ni mapema mno.

Kemikali nyingi zinaweza kuuwa saratani ya matiti katika panya, lakini kuna mengi ya kufanywa kutoka katika utafiti hizo hadi kufikia kiwango ambacho kinaweza kubadili tiba ya ugonjwa huo. **BBC**



Rais wa Belarus, Alexander Lukashenko hana dalili ya kukaa pembeni licha ya shinikizo kuongezeka na kitisho cha vikwazo vya nchi za Magharibi. **PICHA: MTANDAO**

# Macron azuru Iraq

**PARIS,** Ufaransa

RAIS wa Ufaransa, Emmanuel Macron, amewasili jana nchini Iraq kwa ziara rasmi ya kikazi.

Kwa mujibu shirika la habari la serikali ya Iraq, Macron, ambaye alikuwa nchini Lebanon katika kipindi cha siku mbili zilizopita, ziara yake ina lengo la kuanzisha mkakati mpya kwa ushirikiano na Umoja wa Mataifa.

Macron alikataa kutoa ufafanuzi zaidi kutokana na sababu za kiusalama, ingawa alisema Iraq imekuwa katika wakati mgumu.

Kwa mujibu wa kituo cha televisheni cha Iraq al-Sumaria, Rais huyo wa Ufaransa atatumia saa kadhaa nchini Iraq, kukutana na maofisa wa serikali lakini kituo hicho hakikutoa ufafanuzi zaidi kuhusu safari hiyo.

Wakati kundi la Dola la Kiislamu likitajwa kuendelea kuwa na nguvu katika baadhi ya maeneo kadhaa ya Iraq, mwezi Julai, Waziri Mkuu wa sasa Mustafa al-Kadhimi alitangaza kufanyika uchaguzi mkuu wa mapema wa Bunge mwakani. **DW**

# Mgonjwa ajifungua kwenye chopa

**ROME,** Italia

MHAMIAJI mjamzito aliyepatikana na virusi vya corona amejifungua ndani ya helikopta wakati akisafirishwa kwenda hospitali kutoka kwenye kituo cha wahamiaji nchini Italia kilichopo katika kisiwa cha Lampedusa.

Mwanamke huyo ambaye bado hajatambuliwa kwa sasa yuko katika hospitali ya Palermo pamoja na mtoto wake mchanga.

Italia ilisema kuwa imeshuhudia ongezeko la wahamiaji wanaowasili mwaka huu. Meli ya uokozi ilipewa ruhusa Jumanne kuwasafirisha wahamiaji 353 waliookolewa kwenye kisiwa cha Sicily baada ya kupigiwa simu na Umoja wa Mataifa ulioitaka iwaokoe.

Wakati huo huo, meli ya mafuta iliyokuwa na wahamiaji 27 ndani yake imeomba upya isaidiwe kuwafikisha kwenye mwambao wa Italia.

Meli hiyo ya kibiashara, Maersk Etienne, wahusika walisema iliwaokoa wahamiaji hao kutokana na ombi la Malta mapema mwezi Agosti, lakini tangu wakati huo imeachwa baharini.

Wafanyakazi wake walisema watu waliomo wana hali mbaya.

Mwanamke huyo alikuwa amepatikana na virusi vya corona wakati alipopata uchungu wa uzazi.

Kulingana na taarifa za shirika la habari la Reuters, mwanamke huyo alikuwa anaishi katika kituo kinachowashikilia wahamiaji ambacho kilikuwa kimejaa mara kumi ya uwezo wake wa kawaida.

Maofisa walisema waliamua kumuhamishia katika hospitali ya mji mkuu wa Sicily Palermo, uliopo umbali wa mwendo wa saa moja kwa ndege ili aweze kujifungua kwa usalama lakini alijifungua ndani ya ndege.

Tukio hilo limetokea huku kukiwa na mzozo baina ya watawala wa kisiwa cha Sicily na serikali ya taifa, huku Gavana wa Sicily, Nello Musumeci akiishutumu Roma kwa kutompatia msaada wa kutosha wa kushughulikia wahamiaji wanaowasili kutoka Afrika.

Kwa mujibu wa taarifa zilizoangaliwa na shirika la habari la Reuters, hadi sasa tangu mwaka uanze wahamiaji wapatao 19,400 wamewasili kwenye maeneo ya mwambao wa Italia, ikilinganishwa na wahamiaji wapatao 5,200 waliowasili katika kipindi sawa na hicho mwaka jana.

Umoja wa Mataifa ulisema watu zaidi ya 40,000 wamewasili Ulaya kupitia baharini mwaka huu na 443 wamekufa au wamepotea walipokuwa wakijaribu kuvuka bahari ya Mediterranean wakitokea Afrika magharibi. **BBC**



# INTER MILAN YAMWONDOA MARTINEZ SOKONI

**MILAN,** Italia

MKURUGENZI wa Michezo wa Inter Milan, Piero Ausilio, amesema Barcelona ilimtaka Lautaro Martinez lakini straika huyo kwa sasa "hayupo sokoni."

Martinez amekuwa akihusishwa sana na uhamisho wa kwenda Barca tangu mapema mwaka huu, hasa wakati wa kipindi cha mlipuko wa virusi vya corona.

Uvumi huo uliibuka kipindi hicho, huku vyombo vya habari vikidai kwamba Barca inataka kumfanya Martinez kuwa mrithi wa muda mrefu wa Luis Suarez.

Lakini kumekuwa na mtikisiko wa ndani ya Barca kwa kipindi cha miezi kadhaa, hasa baada ya Lionel Messi kuomba kuondoka, huku uvumi wa miamba hao wa Katalunya na Martinez ukiwa kimya.

"Kulikuwa na ofa ya kumtaka mchezaji wetu kutoka Barcelona, lakini hatukuanza majadiliano ya makubaliano," amesema Ausilio akiiambia Sky Sport Italia.

"Lakini kwa sasa tunamchukulia Lautaro kwamba yupo nje ya soko la wachezaji wa kuuzwa."

Aliongeza kusema; "lakini hiyo haina maana kusema kwamba, Inter haitafanya biashara na Barca."

# Nikistaafu nitasema nilimnoa Kroos-Zidane

**MADRID,** Hispania

ZINEDINE Zidane amemwelezea Toni Kroos kama mchezaji wa "aina yake", na atachukulia kama tuzo ya heshima kwake kumnoa nyota huyo wakati atakapostaafu.

Kroos alijiunga na Madrid kutoka Bayern Munich mwaka 2014 na amewasaidia Blancos kushinda mataji mawili ya LaLiga na matatu ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Zidane amemnoa Kroos tangu mwaka 2016 kwa awamu mbili tofauti na kocha huyo wa Madrid hana shaka kwamba mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani atakumbukwa kama kiungo bora zaidi kuwahi kutokea.


"Atakumbukwa kama mchezaji wa aina yake, mmoja wa viungo bora duniani," amesema Zidane akiiambia TyC.

"Wakati nilipowasili nilifurahi sana kuwa kocha wake.

"Ni kweli wakati nitakapostaafu nitakuwa na uwezo wa kusema kwamba niliwanoa Cristiano (Ronaldo), (Gareth) Bale, (Luka) Modric, (Sergio) Ramos. Lakini pia nitasema nilimnoa Toni Kroos.

"Inavutia kumwona akiwa kwenye mazoezi kila siku. Namna gani alivyo na weledi. Kumzungumzia yeye ni kumzungumzia mtu ambaye ni wa aina yake."



# Greenwood ataka kuvunja rekodi England

**LONDON,** England

MASON Greenwood anataka kuvunja rekodi wakati kinda huyo wa Manchester United akijiandaa kuichezea kwa mara ya kwanza Timu ya Taifa ya England.

Greenwood ameitwa kwa mara ya kwanza kwenye kikosi cha England kinachonolewa na kocha, Gareth Southgate kwa ajili ya maandalizi ya mechi za mashindano ya Ligi ya Mataifa ya Uefa dhidi ya Iceland na Denmark.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 18 amejumuishwa kwenye kikosi hicho baada ya kuwa na msimu wa kuvutia pale Old Trafford, ambako alifunga mabao 17 katika mashindano yote kwa United msimu wa 2019-20.

Na Greenwood anaota makubwa kwa England wakati wakijiandaa kucheza dhidi ya Iceland.

"Kwa kawaida mchezaji yeyote kijana anataka kuvunja rekodi," amesema Greenwood na kuongeza; "Na kama utashindwa, kuna kitu kinakuwa hakipo sawa.

"Mara zote ni jambo zuri kuwa na maono na malengo ambayo unayapanga kwenye kipindi chako cha uchezaji soka na hicho ndio ninachokitaka kwenye kikosi cha England.

"Ni kwenda pale na kufanya kazi kwa ubora wangu na kuvunja rekodi ili ukumbukwe milele."

# Van Persie ampigia chapuo Van Gaal

**AMSTERDAM,** Uholanzi

LOUIS van Gaal au Bert van Marwijk wanatakiwa kuwa miongoni mwa wenye nafasi kubwa ya kuchukua mikoba ya Ronald Koeman kama kocha mkuu wa Uholanzi, kwa mujibu wa Robin van Persie.

Koeman alikuwa na wakati mzuri alipoinoa Uholanzi kwa kipindi cha miaka miwili na nusu na kuifikisha fainali ya Ligi ya Mataifa ya UEFA, huku pia akiwapa nafasi ya kuchomoza, wachezaji chipukizi kama Frenkie de Jong na Matthijs de Ligt.

Hata hivyo, Koeman aliachia nafasi hiyo na kwenda Barcelona Agosti, na kuiacha Uholanzi ikitafuta kocha mpya kwa ajili ya mashindano ya Ulaya.

Van Gaal ameinoa Uholanzi mara mbili, mara ya mwisho aliiongoza kwenye nusu fainali ya Kombe la Dunia mwaka 2014 kabla ya kuchukua nafasi ya kuwa kocha wa Manchester United.

Nyota wa zamani wa Oranje hao, Van Persie – mfungaji mwenye rekodi kwa kikosi cha Uholanzi – alicheza chini ya Van Gaal kwa timu zote, ya taifa na United, anaamini kocha huyo mwenye umri wa miaka 69 atakuwa chaguo sahihi.

"Sijawahi kufanya kazi na Ronald Koeman, hivyo siwezi kumhukumu kama kocha," amesema Van Persie akiwa ameandika kwenye kolamu yake katika gazeti la De Telegraaf.

"Nilichojifunza ni kwamba ana mawasiliano mazuri, na naamini atakuwa chaguo sahihi kwa kikosi cha Uholanzi."





# DEPAY: SIJAFIKIRIA KUONDOKA LYON

**LYON,** Ufaransa

MEMPHIS Depay bado ana majukumu ndani ya Lyon, akisisitiza kwamba kamwe hajawahi kuonyesha nia ya kuondoka klabuni hapo.

Depay amekuwa akihusishwa na uhamisho wa kuondoka pale kwenye uwanja wa Groupama, huku Paris Saint-Germain, Inter na Barcelona zikitajwa kumwania fowadi huyo wa zamani wa Manchester United.

Amefunga mabao sita kwa Lyon kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2019-20, akiisaidia Lyon kufika nusu fainali baada ya kuwatoa Juventus na Manchester City. Ameanza vizuri zaidi msimu huu wa 2020-21 kwa kuifungia Lyon mabao matatu 'hat-trick' kwenye mchezo wa kwanza wa Ligi kwa kikosi hicho cha kocha, Rudi Garcia wakati wakishinda 4-1 dhidi ya Dijon.

Akizungumza na NOS, Depay, ambaye mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimi huu, alisema: "Kamwe sijawahi kusema nataka kuondoka. Wakati ninaposema kitu fulani mara nyingine inatafsiriwa tofauti.

"Bado nina mwaka mmoja kwenye mkataba wangu, mimi ni nahodha, na tuna timu nzuri. Tumeonyesha hilo. Najisikia vizuri kuhusu mimi mwenyewe, lakini nina ndoto. Mara zote nimeonyesha hilo."

Kama uvumi wa uhamishi wake wa kwenda Barca utakuwa kweli, utamfanya Depay kuungana na Ronald Koeman, ambaye ameacha nafasi yake kama kocha wa Uholanzi na kuchukua mikoba kule Camp Nou.

# *Arsenal yakamilisha usajili wa Gabriel*

**LONDON,** England

ARSENAL imekamilisha usajili wa mlinzi, Gabriel Magalhaes kutoka Lille, klabu hiyo imethibitisha.

Mlinzi huyo wa kati raia wa Brazil amekubali kusaini mkataba wa muda mrefu na washikabunduki hao na ada yake imeripotiwa kuwa ni euro milioni 30.

"Tunamkaribisha Gabriel hapa Arsenal. Ana ubora mwingi ambao utakifanya kikosi chetu kuwa imara," amesema kocha mkuu, Mikel Arteta. "Amethibitisha hilo akiwa na Lille kwamba ni mlinzi mwenye mchango mkubwa na tunasubiri kumuona yeye akikua kama mchezaji wa Arsenal."

Mkurugenzi wa ufundi, Edu aliongeza: "Tumefurahi kumsajili Gabriel. Yeye ni mchezaji ambaye tumekuwa tukimfuatilia na alikuwa anawaniwa na klabu nyingi, hivyo tunajisikia fahari kwa kuweza kufanikisha usajili wake kutoka Lille.

"Gabriel ni mchezaji mwenye ubora na Mikel na wasaidizi wake wanasubiria kuona ubora wake akiwa na klabu hii."

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 alikuwa nguzo muhimu kwa kikosi cha kocha Christophe Galtier na alicheza mechi 24 kati ya 28 za Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, kabla ya ligi kufutwa kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# SUAREZ AKARIBIA KUTUA JUVENTUS

●●● Ni baada ya Koeman kumweleza hana nafasi kwenye kikosi chake cha Barcelona...

**JUVENTUS,** Italia

KLABU ya Juventus imemtaja Luis Suarez kuwa ni mmoja wa wachezaji bora duniani na anafaa kwenda kuimarisha safu yao ya ushambuliaji.

**Mshambuliaji huyo raia wa Uruguay anatarajia kufikisha umri wa miaka 34 msimu huu na ameelezwa na Kocha mpya wa Barcelona, Ronald Koeman, kwamba hayuko kwenye mipango yake.**

Gazzetta dello Sport na Corriere dello Sport yote yameandika Suarez na Juventus tayari wameshafikia makubaliano ya awali.

Inaeleweka na watatumia faida ya agizo lililowekwa na serikali ya Italia kufuatia kushuka kwa uchumi kwamba mshambuliaji huyo ataweka akiba ya karibu asilimia 50 ya mshahara wake katika kipindi cha miaka miwili.

Kushuka huko kwa uchumi kumepitishwa kutokana na nchi kuyumba baada ya kukumbwa na mlipuko wa virusi vya ugonjwa wa corona (COVID 19), hali ambayo inaweza kusaidia mchakato wa kumsajili Suarez.

Inaelezwa kwamba mshambuliaji huyo ameshafanya mawasiliano na Mkurugenzi Mtendaji wa klabu hiyo, Pavel Nedved, kuhusiana na uhamisho baada ya Koeman kumweleza kwenye simu kwamba hamhitaji kwenye kikosi chake.

Andrea Pirlo anatarajia kufanya mazungumzo na Suarez kwenye simu kuhusiana na uamuzi huo wa kuuzwa na kukamilisha mchakato huo kirahisi, na anatarajia atakuwa mmoja wa wachezaji tegemeo kwake kwa kuonyesha kiwango kizuri sambamba na Lionel Messi na Cristiano Ronaldo.

Inatajwa pia utaratibu wa kusajili wachezaji kwa Juventus umekuwa na mabadiliko katika siku za hivi karibuni.

Klabu hiyo inakaribia kukamilisha usajili wa straika wa Roma, Edin Dzeko lakini bajeti ya timu hiyo bado haijapitisha.

Kumekuwa na sintofahamu inayoendelea lakini ujio wa Suarez unaonekana utakuwa na faida klabuni hapo. Na kwa sasa, Roma na Juventus ziko kwenye nafasi ya kufikia makubaliano ili kukamilisha malengo yao.

Lakini uhamisho wa Suarez unatajwa utakamilika mapema, na unaweza kuchukua siku moja, na Barcelona ikitakiwa kumruhusu na kumlipa pauni milioni 22 kutokana na uamuzi wake wa kutomhitaji tena.

Kama Koeman atatoa ruhusa ya kuvunja mkataba wa mshambuliaji huyo wa zamani wa Liverpool, Pirlo ataongeza nguvu ya kumwania mchezaji huyo na anatajwa kuunda safu hatari ya ushambuliaji kwenye kikosi chake.

Atakuwa na nyota watatu mahiri ambao ni Ronaldo, Suarez na Paulo Dybala, huku pia Dzeko akitajwa kuwa ni mbadala wap, na kuifanya Juventus kuimarisha na kurejea kwenye mbio za kuwania ubingwa wa Serie A ikiwa na kikosi imara.

## ZISIKUPITE

### MESSI, CITY KIMEELEWEKA

MSHAMBULIAJI wa Barcelona, Lionel Messi (33), amefikia makubaliano ya kusaini mkataba wa miaka mitano na Kampuni ya Soka ya City wenye thamani ya pauni milioni 623 ambao utamfanya aitumikie Manchester City kwa misimu mitatu na baadaye atajiunga na New York City FC inayoshiriki Ligi Kuu Marekani. ***(Record)***

### UNITED YAMGANDA SANCHO

MANCHESTER United bado haijakata tamaa ya kuwania saini ya winga wa Borussia Dortmund, Jadon Sancho (20), licha ya nyota huyo wa Timu ya Taifa ya England kutangaza anataka kubakia Ujerumani. ***(Sun)***

### PSG YAMFUATA BELLERIN

PARIS St-Germain imewasilisha ofa ya pauni milioni 25 na nyongeza ya pauni milioni 5 kwa Arsenal ili kumsajili beki wake wa kulia, Hector Bellerin. Beki huyo wa Timu ya Taifa ya Hispania mwenye umri wa miaka 25, anawindwa pia na Bayern Munich na Juventus. ***(Guardian)***

### RODRIGUEZ RASMI EVERTON

EVERTON imefikia makubaliano ya kumsajili kiungo mchezeshaji wa Timu ya Taifa ya Colombia, James Rodriguez (29), akitokea Real Madrid kwa mkataba wa miaka mitatu. ***(Telegraph - subscription required)***

### ALLAN ATUA ENGLAND

KIUNGO wa Napoli Mbrazili, Allan (29), alitarajia kufanya vipimo vya jana ili kukamilisha mchakato wa kujiunga na Everton ambayo inatumia Uwanja wa Goodison Park. ***(Sky Sports)***

### KANTE KUIKAMUA INTER

CHELSEA inahitaji kulipwa pauni milioni 80 ili kumruhusu kiungo wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, N'Golo Kante kujiunga na Inter Milan. Hata hivyo, nyota huyo anapendelea kubakia The Blues. ***(Express)***

### CASTAGNE ATUA LEICESTER

MABOSI wa Leicester City wamekubali kulipa ada ya pauni milioni 22 ili kumsajili beki wa Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Timothy Castagne (24), akitokea Atalanta. ***(Telegraph - subscription required)***

### PARTEY AIVURUGA ARSENAL

NYOTA wa Atletico Madrid, Thomas Partey (27), anajiandaa kujiunga na Arsenal lakini Gunners italazimika kuwatema baadhi ya wachezaji wake ili kulipa ada ya pauni milioni 44 ambayo ni thamani ya raia huyo wa Ghana. ***(Goal)***

### DOUCOURE ANUKIA MONACO

KLABU ya Monaco imeweka wazi nia yake ya kumsajili kiungo Mfaransa wa Watford, Abdoulaye Doucoure baada ya Everton kushindwa kufanikisha mchakato wa kumnasa nyota huyo mwenye umri wa miaka 27. ***(Evening Standard)***

### NDOMBELE AWEKWA SOKONI

KOCHA wa Tottenham Hotspur, Jose Mourinho yuko tayari kumuuza mchezaji aliyeweka rekodi ya kununuliwa kwa fedha nyingi, kiungo wa Ufaransa, Tanguy Ndombele, ambaye alijiunga na klabu hiyo July mwaka jana kwa dau la pauni milioni 53.8. ***(Sun)***

HABARI MICHEZO

## Mwadui yaipigia hesabu Dodoma

Na Shufaa Lyimo

KOCHA Mkuu wa Mwadui FC, Khalid Adam, amewataka wachezaji wake kuongeza bidii kwenye mazoezi ili wajihakikishie namba katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara inayotarajiwa kuanza Jumapili.

Adam alisema hatakuwa na huruma kwa mchezaji ambaye hataonyesha uwezo mzuri uwanjani.

"Sitakuwa na huruma na mchezaji yeyote ambaye hataonyesha ushindani, ndio maana nikasajili wachezaji wapya kwa lengo la kuiongezea timu yangu nguvu," alisema Adam.

Kocha huyo alisema wachezaji wanaendelea vema na mazoezi kwa ajili ya mchezo wao wa kwanza dhidi ya Dodoma Jiji ambao utachezwa kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini humo.

"Tumeweka kambi yetu nje ya Mwadui ili kuepusha kelele za hapa na pale, tulihitaji utulivu zaidi, ninawapa wachezaji wangu mazoezi maalumu ambayo yanahitaji sehemu tulivu," alisema Adam.

Aliongeza kikosi chake kitaanza safari ya kuelekea Dodoma kesho na wanaamini wataanza vizuri msimu mpya kwa kuondoka na pointi tatu huku pia wakiwaheshimu wapinzani wao.

"Wachezaji wangu wananipa matumaini, nidhamu ya kila mchezaji ipo juu, tunawaomba mashabiki wetu wazidi kutuunga mkono kama walivyotufanyia msimu uliopita," kocha huyo alisema.

## Msanii mzalendo atunukiwa cheti

Na Sabato Kasika

MSANII wa muziki wa asili na kizazi kipya, Mohamed Mwampogwa "Mwalimu Pogwa Mzalendo" ametunukiwa cheti cha heshima na fedha taslimu Sh. milioni 1.5 kutokana na kuhamasisha masuala ya kielimu na uzalendo jijini, Tanga.

Mwalimu Pogwa Mzalendo pia amekuwa akitoa sehemu ya mshahara wake kwa ajili ya kusaidia watoto wenye uhitaji.

Msanii huyo ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Jukwaa la Walimu Wazalendo Mkoa wa Tanga, ametunukiwa cheti hicho na mgombea udiwani wa Kata ya Msasa, Hussein Omari, ambaye anayetetea kiti hicho kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM).

"Ninamshukuru diwani kwa kuthamini ninachokifanya, ninamwombea kwa Mungu na ninamwahidi kuwa nitaongeza juhudi katika kutumia vipaji vyangu vyote kuhamasisha masuala ya kizalendo mkoani Tanga na Taifa kwa ujumla," alisema Mwalimu Pogwa Mzalendo.

Kwa upande wake diwani huyo alisema, anamwona msanii huyo kama kijana ambaye ni mfano jijini humo kwa sababu anavyojituma kufanya kazi kuhamasisha masuala ya kielimu na uzalendo.

"Nimemuunga mkono katika juhudi zake hizo akiwa tayari ameingia studio na kurekodi nyimbo zaidi ya 10. Binafsi ninathamini jitihada zake za kuisaidia serikali kuhamasisha vijana wengine wa Tanga kutanguliza uzalendo katika maisha yao bila kujali wanapitia mazingira gani," alisema Omari.

# YANGA PRINCESS YALIPA KISASI SIMBA QUEENS

Na Saada Akida

BAADA ya kuchukuliwa mchezaji wao na mabingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania, Simba Queens, watani zao Yanga Princess wamejibu mapigo kwa kumsajili nyota wa Wekundu wa Msimbazi, Tabea Munga, imeelezwa.

**Yanga ilifanikisha kunasa saini ya Munga katika siku ya mwisho ya kufunga dirisha la usajili kwa ajili ya msimu mpya wa 2020/21.**

Kama ilivyo kwa kaka zao, Simba iliibomoa Yanga kwa kumsajili kiungo wake mahiri, Shelda Boniface, ambaye amerejea katika kiwango chake baada ya kupona jeraha la goti lililokuwa linamsumbua.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Yanga Princess, Edna Lema, alisema wanajipanga imara kuhakikisha wanatwaa ubingwa au kumaliza kwenye nafasi tatu za juu kwenye Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania msimu huu.

Lema alisema wamefanyia kazi mapungufu waliyokuwa nayo katika msimu uliopita kwa kusajili wachezaji kwenye idara zilizokuwa na shida na wanaamini watafikia malengo waliyonayo.

Alisema baada ya kufunga usajili kwa mchezaji huyo sasa wapo kwenye maandalizi ya msimu mpya, na hasa kufuta 'uteja' wa kufungwa kwa misimu mitatu na kwa watani wao wa jadi.

"Tumeboresha kikosi chetu kwa kufanya usajili wa kiwango cha juu, sasa tunaanza maandalizi ya ligi, tumejipanga kwa kufanya programu mbalimbali zitakazowaimarisha wachezaji wetu, tumedhamiria kuleta ushindani mkubwa msimu huu, tunahitaji kutwaa taji la ubingwa na pia kufuta uteja kwa Simba," alisema kocha huyo.

Aliongeza kuwa kikosi chake kitacheza mechi mbalimbali za kirafiki ili kujiimarisha na wanaamini timu zitakazopanda daraja pia zitaongeza ushindani kwenye Ligi Kuu ya Wanawake.




Wachezaji wa Transit Camp inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza wakifanya mazoezi kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam kwa ajili ya kujiandaa na msimu mpya wa 2020/21. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mtibwa yajivunia wachezaji wapya

Na Adam Fungamwango

ILI kufikia malengo yake, Kocha Mkuu wa Mtibwa Sugar, Zuberi Katwila, amesema anawataka wachezaji wapya waliosajiliwa katika timu hiyo kuhakikisha wanatoa mchango mzuri kwa ajili ya kutimiza malengo.

Msimu uliopita, Mtibwa Sugar yenye maskani yake Turiani, Morogoro, haikuwa na msimu mzuri.

Katwila alisema wamefanya usajili kwa kuzingatia uwezo wa wachezaji na mapungufu waliyokuwa nayo kwenye kikosi chao.

"Sisi hatukusajili tu. Tumesajili wakati ligi inaendelea, kwa hiyo tulikuwa tukiviona vipaji na uwezo wa wachezaji wakati mechi zinaendelea, tukajua tukimchukua fulani na fulani wanaweza kufaa na kuingia haraka kwenye mfumo wetu, hivyo tuna imani yao na tunajivunia pia," alisema Katwila, mchezaji wa zamani wa timu hiyo.

Kocha huyo alisema baada ya kuwaona walipeleka majina yao kwa viongozi ambao walifanikiwa kuwasajili na sasa wanachotarajia kutoka kwao kama walivyokuwa msimu uliopita.

"Labda mtu mwenyewe tu ashindwe kuzoea mazingira ambayo yamebadilika kutoka kwake, lakini kila kitu kiko sawa na tuko tayari kwa ligi," Katwila alisema.

Katwila aliwataja nyota wapya waliotua klabuni hapo ni pamoja na Geofrey Luseke, Hamad Hilika, Aboubakar Ame, Kassim Khamisi, Hassan Kessy na Abdul Haule ambaye amepandishwa kutoka kikosi cha vijana.

Michezo
Alhamisi Septemba 3, 2020
Nipashe




Suarez akaribia kutua Juventus UKURASA 22

# SIMBA, YANGA KATIKA KITIMOTO

**Ni mpango mkakati ulioandaliwa na Azam kwenye mbio za kuwania ubingwa...**

**Na Saada Akida**

VITA ya kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2020/21 inatarajiwa kuwa kali kutokana na benchi la ufundi la Azam FC kutamba haitarudia makosa waliyofanya msimu uliopita na kueleza wanataka kushinda taji hilo ili washiriki mashindano ya kimataifa.

**Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam, Kocha Msaidizi wa Azam FC, Vivier Bahati, alisema wamejipanga vema na wana mikakati imara kuhakikisha wanapigania ubingwa wa ligi ambao pia unawaniwa na klabu kongwe za Simba na Yanga, zote za jijini.**

Bahati alisema timu yake inakiu na taji hilo ambalo waliwahi kulichukua mara moja katika msimu wa 2013/14 na sasa wanafikiri ni wakati sahihi kurejea klabuni hapo.

"Tumejipanga imara, tumeyafanyia kazi mapungufu ya msimu uliopita, tumekuwa na maandalizi mazuri, kwa kifupi tunahitaji kushinda taji la Ligi Kuu Tanzania, tumedhamiria kuusaka ubingwa kwa udi na uvumba," alisema Bahati.

Kocha huyo aliongeza usajili waliofanya umelenga kuwania ubingwa na ulifuata mapendekezo ya ripoti ya kiufundi waliyoiwakilisha kwa viongozi baada ya kumaliza msimu uliopita.

Alisema viongozi walikamilisha majukumu yao kwa upande wa utawala na kazi imebaki kwao wachezaji na benchi la ufundi kuhakikisha malengo yanatimia.

"Tunaendelea na programu ya mazoezi tuliyoiandaa, inakwenda vizuri kwa sababu tunataka kuhakikisha tunapata matokeo mazuri katika michezo yetu yote ya ligi ya msimu huu, najua itakuwa ni ligi yenye ushindani mkubwa, kwa sababu kila timu imejipanga na kujiimarisha vizuri," Bahati alisema.

Aliongeza ameridhishwa na viwango vya wachezaji wao wote waliosajiliwa kwa ajili ya msimu mpya, lakini matokeo ya mechi za tatu za kirafiki walizocheza yamewapa picha ya mwelekeo wao.

"Kikosi chetu kimekamilika, kama tutafanya kile tunachokitarajia, msimu huu utakuwa mzuri kwetu, tumejipanga na kujiimarisha katika kila idara, tunaomba wachezaji wawe watulivu na kufuata maelekezo, tumewasoma wapinzani wetu wa karibu, hawatatusumbua tena," alisema kocha huyo.

Aliongeza wachezaji wa Simba na Yanga wamekuwa wakipewa sifa zaidi, lakini kwa uhalisia, msimu huu, Azam FC imesajili vema na wanatarajia kupata mataji mbalimbali kwenye mashindano watakayoshiriki.

Katika kujiandaa na msimu mpya, Azam FC ilipata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Namungo ya Lindi halafu ikawafunga KMC bao 1-0 na vile vile ililazimishwa sare ya goli 1-1 dhidi ya Tanzania Prisons, mechi zote zikichezwa Uwanja wa Azam Complex.

Azam FC wataanza msimu wa 2020/21 nyumbani kwa kuwakaribisha Polisi Tanzania kutoka Kilimanjaro, Moshi wakati mabingwa watetezi watakuwa ugenini Mbeya kuwakabili Ihefu huku Prisons wakiwafuata Yanga kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini.




Kiungo mshambuliaji wa Simba, Bernard Morrison (kulia), na Larry Bwalya wakipambana kuwania mpira katika mazoezi ya timu hiyo inayojiandaa na mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Ihefu FC yaliyofanyika kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya jana asubuhi. **PICHA: MTANDAO**

## Kishindo kizito, Simba na Ihefu

**Na Faustine Feliciane**

TUKO safi! Hayo ni maneno kutoka kwa Meneja wa mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, Patrick Rweyemamu, kuelekea mechi ya kufungua pazia la msimu mpya dhidi ya Ihefu FC itakayochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Sokoine jijini, Mbeya, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Rweyemamu, alisema wachezaji wa timu hiyo wako katika hali nzuri na wanajipanga kuanza vema kutetea ubingwa wanaoushikilia.

Rweyemamu alisema hakuna majeruhi aliyeongezeka katika kikosi chao na hali ya David Kimeta inaendelea vema.

"Kikosi kinaendelea vizuri kwa kweli, tunashukuru leo (jana) asubuhi tumefanya mazoezi yetu ya kwanza tangu tufike huku (Mbeya), na pia tutafanya jioni, kila mchezaji yupo katika hali nzuri ukimwondoa Kameta peke yake," alisema Rweyemamu.

Alisema wachezaji wote wameelekeza nguvu na akili yao kwenye Ligi Kuu Bara na wanashangazwa na taarifa za ugomvi kutokea kwenye kambi yao kati ya mshambuliaji, Meddie Kagere na kocha, Sven Vandenbroeck.

"Watu wanasema ugomvi huo umetokea mazoezini, tunajiuliza mazoezi yapi wakati sisi tangu tufike huku hatujafanya mazoezi, hizi habari za kutengenezwa na hazina tija yoyote, hawatuondoi kwenye malengo yetu," alisema Rweyemamu.

Aliongeza wanatarajia kuanza ligi kwa kishindo na wamepanga kutimiza malengo yote waliyojiwekea ya kufanya vizuri zaidi msimu huu.

"Ndani ya kambi yetu huku Mbeya kila mmoja ameelekeza mawazo yake kwenye mchezo ulioko mbele yetu, tunataka kuanza kwa kishindo," aliongeza Rweyemamu.

Baada ya mechi ya Jumapili, Simba itaelekea Morogoro kuwafuata Mtibwa Sugar katika mechi ya raundi ya pili itakayochezwa Septemba 12, mwaka huu kwenye Uwanja wa Jamhuri mkoani humo.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042